# Nipashe

Jumamosi Februari 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580490

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11

**Ajali** bodaboda ilivyokatisha uhai wa diwani

UKURASA 2



**Watendaji** waingia matatani tuhuma kula fedha mbichi

UKURASA 4

# JPM: Mawaziri hawa nitafukuza

UKURASA 2



## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### MAGUFULI APONGEZA UTENDAJI WA ABOOD

RAIS John Magufuli, amempongeza Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (CCM), kutokana...

**UKURASA WA 5**

### RC ATAKA MAOFISA TRA KUJITATHMINI

MKUU wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, amewataka maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania...

## Katibu CCM Morogoro asimamishwa madai ya rushwa

UKURASA 3



Baadhi ya wabunge wakipokea kwa masikitiko taarifa ya Spika wa Bunge, Job Ndugai (hayupo pichani), Bungeni jijini Dodoma, kuhusu kifo cha Mbunge wa Muhambwe, Atashasta Nditiye (picha ndogo), aliyefariki jana asubuhi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, baada ya kupata ajali. **PICHA: OWM**



## Mchango wa mwisho wa Nditiye bungeni ni huu



UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store

**MICHEZO** **YANGA 'KUVUNJA MWIKO' MBEYA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Magufuli: Mawaziri hawa nitafukuza, wasinilaumu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

RAIS John Magufuli amewataka mawaziri na watendaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji, kuhakikisha kunakuwa na spidi katika uanzishwaji wa viwanda nchini, vinginevyo atawafukuza na wasimlaumu kwa uamuzi huo.

Amesema wizara hizo zimekuwa zikifanya ucheleweshwaji na kuzungusha wawekezaji ili watoe rushwa wakati Watanzania wanahitaji viwanda kwa ajili ya kujipatia ajira na maendeleo.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua kiwanda cha uchakataji wa mazao jamii ya mikunde na viungo cha Mahashree Agro Processing Tanzania Limited kilichoko Mikese Wilaya ya Morogoro.

"Tumechelewa sana, lakini unakuta mwekezaji anajitokeza kutaka eneo la kuanzisha kiwanda, watendaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji wamekuwa hawataki kuharakisha mambo mpaka wahongwe. Sasa wasipobadilika nitawafukuza kwani watu wanataka matokeo," alionya.

Rais Magufuli alisema endapo viongozi na watendaji wa wizara hizo alizozitaja hawatabadilika na kupeleka mambo kwa spidi katika uanzishwaji wa viwanda, atawafukuza bila kuangalia sura zao kwa kuwa kila siku anaombewa na viongozi wa dini.

Alisema nia ya serikali ni kuona viwanda vinajengwa kwa wingi na kuwataka Watanzania wenye uwezo kujenga viwanda hivyo na wasiogope kuitwa mafisadi huku akihamasisha viongozi wa vyama vya siasa, dini na wabunge kujitokeza kuanzisha viwanda.

"Usiogope kuanzisha kiwanda kwa sababu kuitwa fisadi. Uwe ni mfanyakazi, uwe mbunge, uwe kiongozi wa dini, uwe sheikh, uwe diwani, uwe askofu, anzisheni kiwanda. Nitafurahi siku moja Baba Askofu Mkude anialike kuja kufungua kiwanda chake," alisema.

Rais Magufuli alisema kwa sasa ni lazima mawazo yote ya Watanzania wote kwa pamoja kuyapeleka katika kutengeneza pesa kutokana na kuanzisha viwanda nchini, ambavyo vitatoa ajira kwa wananchi.

Alisema suala la ujenzi wa viwanda hivi sasa siyo la serikali bali ni la watu binafsi ndiyo nafasi zao na kwamba atafurahi siku moja kuona chama chake kinamwalika kwenda kufungua kiwanda kilichojengwa na CCM na vyama vingine kama CHADEMA, ACT- Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF) wanamwalika kwenda kufungua viwanda vyao.

Akizungumzia kiwanda hicho cha Mahashree Agro Processing Tanzania Limited, Rais Magufuli alisema ni mfano wa kuigwa kwa kuwa kitawasaidia kutoa ajira na kuwasaidia wakulima kwa kuingia mikataba ya kuuza mazao yao yalikuwa yanakosa soko.


Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Murk Mahashree, alisema hadi kufikia mwaka 2023, wanatarajia kuingia mikataba na wakulima 14,000 na kupitia mkataba huo, watakuwa na soko la uhakika wa mazao wanayozalisha.

Alisema ili kupata mazao yenye ubora na kuongeza uzalishaji, wamejipanga kuwatumia wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ili kupitia utaalamu wao, wakulima waongeze uzalishaji wenye tija kwa mazao hayo na yanayokubalika katika masoko ya nje.

Alisema mbali na kujenga kiwanda hicho, pia wanakusudia kuanzisha kiwanda cha sukari kutokana na mazingira bora ya ardhi iliyopo nchini na kuiomba serikali kuwapatia eneo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema wizara imejipanga kushirikiana na uongozi wa kiwanda hicho ili kuona njia bora ya kuimarisha masoko katika nchi 14.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema katika awamu ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano, viwanda 8,477 (vikubwa 201, vya kati 460, vidogo 3,406 na vidogo kabisa 4,410) vimeanzishwa.



Rais Dk. John Magufuli akikata utepe kuzindua kiwanda cha ngozi cha Taifa cha Ace Leather Industries, katika eneo la viwanda la Mahonda, mjini Morogoro jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Rostam Azizi na (kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare. **PICHA: IKULU**

## Bodaboda ilivyokatisha uhai wa diwani

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

DIWANI wa Ligoma, Tarafa ya Namasakata wilayani Tunduru mkoani Ruvuma (CCM), Abbas Ngajime (61), amefariki dunia kutokana na ajali ya pikipiki.

Mashuhuda wa tukio hilo, wamedai Ngajime alipata ajali hiyo katika eneo la barabara ya kuelekea Bomani kutoka mjini Tunduru na kwamba chanzo cha ajali hiyo diwani huyo kuingia barabara kubwa bila tahadhari.

Walisema jana kuwa Ngajime aligongwa na pikipiki na kukimbizwa katika Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya matibabu.

Walisema ajali hiyo ilitokea katika aneo hilo kutokana na mwendokasi aliokuwa akiendesha dereva wa pikipiki, aliyeshindwa kukimudu chombo chake.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, akibainisha kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:30 jioni.

Alisema katika tukio hilo, Ngajime alikuwa anatumia pikipiki yake aina ya SLG yenye namba za usajiri T 149 AUF na kuongeza kuwa taarifa zinaonyesha kila mmoja kati yao alikuwa akikimbia mvua ambayo wakati huo ilionekana kuanza kunyesha.

Alisema kuwa baada ya tukio hilo, dereva mwenzake ambaye hakuweza kufahamika, alikimbia na kutokomea kusikojulikana, lakini Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka dereva huyo ili sheria ifuate mkondo wake.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi ambao wanazo taarifa za eneo alikokimbilia na kujificha dereva huyo, kulisaidia Jeshi la Polisi ili akamatwe.

Kamanda Maigwa aliwataka madereva kuzingatia usalama wa maisha yao na waenda kwa miguu pindi wanapokuwa wanaviendesha vyombo vyao ili kuokoa maisha yao na kuepuka kusababishia ulemavu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gasper Balyomi, alisema Ngajime alifariki dunia akiwa katika Hospitali ya Missioni ya Ndanda wakati jitihada za kumwahisha katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa ajili ya matibabu ya kibingwa zikiendelea.

Alisema Ngajime alikuwa anakimbizwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili zikiwa ni juhudi za kuokoa uhai wake baada ya maofisa tabibu wa Hospitali ya Wilaya kubaini alikuwa anahitaji matibabu ya kibingwa.

Alisema taarifa za maofisa tabibu wa hospitali hiyo zilionyesha Ngajime aliumia vibaya sehemu za kichwani na kuvunjika mara mbili mguu wa kulia.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Haillu Mussa, alisema mwili wa mwanasiasa huyo utazikwa kwa heshima zote inavyostahili.

HABARI KITAIFA

# Magufuli: Katibu CCM Morogoro amesimamishwa kazi kwa rushwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, ametangaza kusimamishwa kazi kwa Katibu wa chama hicho Mkoa wa Morogoro kutokana na tuhuma za kula rushwa kwa madiwani wa Manispaa Morogoro.

Alitangaza uamuzi huo alipowahutubia wananchi wa Manispaa ya Morogoro baada ya kuzindua rasmi Soko Kuu la Morogoro alilolipa jina la Chifu Kingalu.

Alisema Katibu wa CCM wa Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu, amesimamishwa kazi na atajadiliwa kwa kuwa anatuhumiwa kula rushwa kwa madiwani.

"Hata wewe meya ninataka ubadilike, ninajua umeupata umeya wa bahati, hukutakiwa kuwa meya. Aliyetakiwa sikumrudisha kuwa meya," alisema huku akishagiliwa na wananchi waliokuwapo kwenye hafla hiyo.

Alisema mchakato wa utafutaji wa meya katika Manispaa ya Morogoro uligubikwa na rushwa ndiyo maana wakaamua kumsimamisha kazi Katibu wa CCM, ili kujadiliwa katika vikao vya chama hicho.

"Sasa, na wewe kwa sababu umeupata umeya simamia kazi, usimamie hawa wanyonge na ninyi madiwani wenzangu, simamieni haki kwa watu waliowapigia kura.

"Udiwani ni utumishi, hamwezi mkawa mnapitisha sheria ndogo za kuwaumiza wale watu waliowapigira kura. Kazi ya ubunge, kazi ya udiwani ni utumishi na ni lazima kuubeba kuwatumikia wanyonge."

Novemba 23, mwaka jana, kulifanyika uchaguzi wa meya wa Manispaa ya Morogoro na Seifu Chomoka akipata kura 20, Pascal Kihanga 11 na Khamis Ndwata 11.

Kutokana na matokeo hayo kumpa ushindi Chomoka, wagombea wawili waliopata kura chache, waliandika barua ya kukata rufani kwa Kamati ya Siasa na kufika kamati kuu kupinga ushindi huo wa Chomoka kwa madai haukifikia nusu ya kura zote na baadaye kamati kuu kuagiza uchaguzi urudiwe.

Kamati Kuu ya CCM Taifa ikaagiza uchaguzi kurudiwa na Januari 12 mwaka huu, ukafanyika kwa wagombea Seifu Chomoka kupata kura 21 na Pascal Kihanga kupata kura 20, huku Ndwata akipatakura moja.

Hata hivyo, uchaguzi huo ulirudiwa tena kwa Chomoka na Kihanga na wakafungana kwa kupata kura 21 kila mmoja, na majina yao yaliamuliwa kupelekwa Kamati Kuu ya CCM Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

Uamuzi wa kamati hiyo uliotangazwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanania Bara, Roderick Mpogoro, ulirejesha jina la Kihanga kuwa Meya wa Manispaa ya Morogoro.

# Mchango wa mwisho Nditiye bungeni

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

MBUNGE wa Mhambwe mkoani Kigoma (CCM), Atashasta Nditiye (52), amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Kibingwa ya Benjamin Mkapa (BMH) baada ya kupata ajali.

Nditiye aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, alipata ajali katika eneo la Nanenane jijini Dodoma Februari 10 na alifikwa na umauti jana majira ya saa nne asubuhi wakati akipatiwa matibabu.

Huyo ni mbunge wa pili kufariki dunia katika Bunge la 12 lililoanza Novemba 13 mwaka jana.

Januari 21, mwaka huu, Bunge lilimpoteza aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Martha Umbula (CCM), aliyefariki dunia India, alikokuwa akiendelea na matibabu.

Jana, Spika wa Bunge, Job Ndugai, akitangaza kuahirisha shughuli za Bunge hadi leo asubuhi, alisema kabla ya kifo, Nditiye alipata ajali Februari 10 mwaka katika eneo la Nanenane jijini na kukimbizwa kupatiwa matibabu ya awali Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

"Kwa masikitiko makubwa, nichukue fursa hii kutangaza kwamba mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye, amefariki dunia leo (jana) ijumaa tarehe 12 Februari 2021, saa nne asubuhi Hospitalini Benjamini Mkapa alikokuwa akipata matibabu.

Kanuni ya 173 ya Bunge inataka kuahirisha shughuli za Bunge kunapotokea kifo cha mbunge wakati Bunge likiwa kwenye shughuli zake.

Kwa kuzingatia kanuni hiyo, Spika Ndugai alitangaza: "Sasa, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho (leo) Jumamosi Februari 13 saa 3:00 asubuhi ili waheshimiwa tupate taarifa zaidi kuhusu namna tutakavyomuaga mbunge mwenzetu zitatolewa baadaye.

"Ninaomba wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane wote Ukumbi wa Spika."

Baada ya kipindi cha maswali na majibu kumalizika, Mbunge wa Kalambo (CCM), Josephat Kandege na Mbunge wa Handeni Vijijini (CCM), John Salu, waliomba mwongozo wa Naibu Spika, wakitaka Bunge liahirishwe kutokana na kuwapo kwa tetesi za msiba huo.

Hata hivyo, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliendelea na ratiba ya mjadala, akisisitiza kuwa bado kiti kilikuwa hakina taarifa rasmi za msiba huo.

"Ninawaomba waheshimiwa wabunge, tutulie na tuendelee na mjadala kwa kuwa kiti hakina taarifa rasmi lakini kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, taarifa nzito kama hii inatolewa na Spika wa Bunge na ameniandikia hapa kuwa anafuatilia katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, atakuja kutueleza taarifa sahihi," alisema Dk. Tulia.

**MCHANGO WAKE WA MWISHO BUNGENI**

Katika mchango wake wa mwisho bungeni, Nditiye alisema: Kumekuwa na maelezo mengi ya waheshimiwa wabunge kwa ujumla ya kuelezea jinsi ambavyo hawaridhiki na pesa iliyotengwa kwa ajili ya TARURA na wakapendekeza kwamba tuangalie uwezekano wa kuchukua hatua ya kuongozea fedha kutoka TANROADS.


"Ninaomba nitoe ushauri, kwanza kabisa hakuna kosa kubwa tutakalolifanya kama tutajaribu kuondoa hiki kidogo walichonacho TANROADS kwa namna yoyote ile.

"Isipokuwa kitu ambacho tunaweza kukifanya ni kuhakikisha tunatafuta vyanzo vizuri na sahihi kwa ajili ya TURURA.

"Sote tunajua umuhimu wa TARURA kwa barabara zetu kuanzia vijijini mpaka barabara kuu na tunajua jinsi wanavyohangaika kutokana na bajeti yao kuwa ndogo.

"Mimi nimeona nije na mpango na niutoe kwa Waziri wa Fedha auangalie kuona kama unafaa. Mwaka jana kipindi kama hiki, nilihudhuria Kamati ya Bunge ya Bajeti na nikatoa kama proposal juu ya jinsi gani tunaweza kuitumia Sekta ya Mawasiliano kuhakikisha tunapata pesa za kutosha kuhakikisha TARURA inafanya shughuli zake kwa wananchi wa Tanzania.

"Kipindi hicho ambacho bado ninasimamia kwenye wazo langu hilo, niliwashauri watu wa kampuni za simu kwamba tuongee na kampuni za simu tuweke tozo kidogo kabisa itakayowezesha TARURA kupata pesa.



"Tukawapa pendekezo kwamba tukiwekeza senti 25 kwa kila megabite moja, sasa hivi Watanzania wanaosajiliwa kwa kutumia laini za simu wapo milioni 50.

"Kati ya watu milioni 50, watu milioni 24 imesomeka kwamba wanatumia mitandao ya intaneti kwa njia mbalimbali na shughuli mbalimbali.

"Mimi nikasema tuchukue tu sampuli ya watu milioni 10, tusichukue wote milioni 24, tuchukue milioni 10 ambao wanatumia intaneti, nikasema tuweke tozo ya senti 25 isifike hata Sh. moja kila megabite moja, nikasema kwa kila gigabite moja ambayo ni 1,000 tukiweka tutakuwa tumeichangia serikali Sh. 250 kwa kila gigabite moja.

"Niliendа mbali zaidi, nitawasilisha hili kwa njia ya maandishi, ninajua itasaidia serikali. Kwanza kabisa, niwahakikishie tusiwe waoga, hizi kampuni za simu zimekuwa na ushirikiano mzuri sana na serikali na zimekuwa zinachangia sana kwenye serikali na hawawezi kulalamika na isitoshe hakuna bei moja ya mtandao mmoja kwenda mwingine katika kutoa huduma kwa wateja wake.

"Tukitoa senti 25 kwa watu milioni 10 ambao kila mmoja anatoa Sh. 250 tufanye kwa wiki moja mtu atatumia gigabite moja, tutakuwa tumetenegeza Sh. bilioni 2.5.

Ukichukua hiyo hesabu kwa muda wa mwezi ni Sh. bilioni 10 na kwa mwaka bilioni 120. Katika hizo bilioni 273 za TARURA, tutakuwa tumewaongezea kiasi kikubwa cha pesa.

**WASIFU**

Nditiye alizaliwa Oktoba 17 mwaka 1969 na aliingia kwenye siasa wakati akiwa mwanafunzi wa Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam (FTC) mwaka 1990 akiwa mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwaka 2017, aliteuliwa na Rais, Dk. John Magufuli kuwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, akimsaidia aliyekuwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa ambaye baadaye alihamishiwa Wizara ya Maji.

Amekuwa Mbunge wa Muhambwe tangu mwaka 2015 hadi umauti unamfika, ukiwa ni mwaka wa sita kuliongoza jimbo hilo ambalo kabla yake, lilikuwa chini ya uwakilishi wa Felix Mkosamali (NCCR-Mageuzi).

Ajira yake ya kwanza ilikuwa katika Kituo cha Mafunzo ya Ufundi tawi la Kigoma, akiwa Msaidizi wa Ufundi Umeme Kuanzia mwaka 1991 hadi 1992.

Historia ya mbunge huyo kielimu inaonyesha alisoma Shule ya Msingi Kabwigwa kuanzia mwaka 1975 hadi 1981 na baadaye alijiunga na Dar es Salaam Technical College ambako alisoma kuanzia mwaka 1984 hadi 1986 na kutunukiwa cheti cha uhandisi.

Mwaka 2008, alitunukiwa Shahada ya Uhandisi wa Umeme na Mawasiliano ya Simu katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na baadaye kuanzia mwaka 2011 hadi 2013 alitunukiwa Shahada ya Uzamili (MBA) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

# JPM apongeza utendaji wa Abood

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

RAIS John Magufuli, amempongeza Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (CCM), kutokana na uzalendo wake katika kusaidia wananchi wa mkoa wa huo.

Kiongozi huyo wa nchi alitoa pongezi hizo juzi, wakati wa ufunguzi wa Soko Kuu la Morogoro.

Rais Magufuli alisema kuwa mbali na kusaidia wananchi, Abood amekuwa akichochea maendeleo hasa kwa wananchi wa hali ya chini wakiwamo wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga na mamalishe kwa kuwapatia mitaji na kuwasemea kero zao.

Awali, Abood alimshukuru Rais Magufuli kwa kuipatia Manispaa ya Morogoro miradi mingi ukiwamo wa maji wa Kihonda-Lukobe wenye thamani ya Sh. bilioni 2.2.

Mbunge huyo alisema mpaka sasa serikali imeshatoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya mradi huo na kumwomba Rais Magufuli kuwawezesha upatikanaji wa kiasi cha fedha kilichobaki cha Sh. bilioni 1.1 ili kumalizia mradi huo muhimu kuwahudumia wananchi wa kata za Lukobe na Kihonda na wasafiri watakaotumia reli ya mwendokasi.

"Mheshimiwa Rais, kwanza tunashukuru kwa miradi mikubwa uliotupatia sisi wakazi wa Manispaa ya Morogoro ikiwamo ya maji, lakini bado zile fedha hazijatoka zote kwa ajili ya kumalizia, hivyo tunaomba usukume jambo hilo ili tukamilishe mradi wa maji kwa kuwa pia utasaidia wasafiri wa reli ya mwendokasi ambayo inakaribia kufunguliwa," alisema.

Mbunge wa Morogoro Kusini, Innocent Karogeles, alikumbushia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010- 2015 na 2015-2020 inayotilia mkazo ujenzi wa barabara ya Bigwa-Kisaki kwa kiwango cha lami.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alizungumzia ucheleweshwaji wa barabara ya Kidatu -Ifakara ulioanza mwaka 2018.

"Mara kadhaa nimefanya mawasiliano na Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Fedha kwa ajili ya barabara hiyo ili kuona ukamilishaji wake, lakini bado kuna kusuasua, ni barabara muhimu kwa uchumi wa wilaya hizo na taifa hivyo tunaomba Rais kuona namna ya kukamilisha," alisema.

Pia, alikumbushia ombi maalum la kupatiwa fedha kwa ajili ya kujenga hospitali ya mkoa kutokana na iliyopo hivi sasa kuwa na hadhi ya wilaya na hivyo imelemewa katika utoaji wa huduma za afya.



Rais Dk. John Magufuli, akikata utepe kuzindua rasmi soko jipya la Mkoa wa Morogoro, ambalo limepewa jina la Chifu Kingalu, juzi. Watatu kulia ni Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (kushoto), Mkuu wa Mkoa huo, Loata Ole Sanare (wapili kushoto) na Mbunge wa Jimbo la Morogoro, AbdulAziz Abood. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# RC aahidi kushughulikia kero za uzalishaji nyuki

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa Pwani, Evarist Ndikilo, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya Mkuranga kwa kushika nafasi ya 10 kitaifa kwa ubora wa asali.

Pongezi za kiongozi huyo wa mkoa ziliwasilishwa na Ofisa Misitu Mkoa wa Pwani, Felix Shayo, aliyemwakilisha mkuu wa mkoa kwenye maadhimisho ya mwaka mmoja wa programu ya 'Nyuki ni Fursa Tuitumie' yaliyofanyika juzi mjini Mkuranga.

Katika hotuba yake iliyowasilishwa na ofisa huyo, Ndikilo alisema serikali inatambua vikwazo vya uharibifu mazingira, watumishi wachache wa sekta hiyo na vitendea kazi ambavyo kwa pamoja vinatafutiwa ufumbuzi.

Alimwagiza Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, kusimamia upandaji miti, uhifadhi mazingira na uundaji vikundi ili mkoa huo ufikie nafasi ya juu zaidi katika uzalishaji wa asali bora huku akiahidi kutoa ushirikiano kutatua vikwazo vilivyopo.

Akisoma taarifa ya wilaya, Ofisa Nyuki, Asted Mpita, alisema wazo la halmashauri ya wilaya ni kuwa na kampeni ya Programu ya Nyuki ni Fursa Tuitumie', inachangia kuhamasisha utalii, akiomba wadau kutengeneza mizinga kwa wingi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Mshamu Munde, alisema kuongezeka misitu ni ishara ya ufanisi wa kampeni hiyo, akiahidi kuunga mkono kuendeleza misitu ambayo ina faida nyingi.

Munde alisema kampeni hiyo itaimarishwa ili itumike kuongeza mapato ya halmashauri ya wilaya na serikali kuu kwa ujumla.

Mkuu wa Wilaya, Filberto Sanga, aliipongeza halmashauri kuandaa hafla hiyo na kuipa kipaumbele huku akiagiza iwe endelevu wajikomboe kiuchumi.

Sanga aliyewakilishwa na Katibu Tawala wa Wilaya, Veronica Kinyemi, alisema kampeni hiyo inatakiwa kuendelezwa ili wananchi waelewe njia na faida za ufugaji nyuki na kufaidika na fursa ya kujiajiri na kutafuta masoko ya uhakika.

Katika hafla hiyo, wadau mbalimbali walipewa tuzo akiwamo Mkurugenzi wa Halmashauri, Munde, ambaye ofisi ya nyuki ipo chini ya uratibu wake.

# Watendaji matatani kwa tuhuma kula fedha mbichi

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

MKUU wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, Carlolius Misungwi, ametoa siku 16 kwa watendaji wa kata na vijiji kuhakikisha wanarejesha Sh. milioni 162 ambazo ni makusanyo ya halmashauri hiyo ambazo wanadaiwa kuzitumia kwa matumizi yao binafsi.

Amesema wakishindwa kurejesha fedha hizo, watakamatwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Misungwi alitoa agizo hilo jana kwenye kiako cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo lililoketi kwa ajili ya kupitisha mpango na bajeti ya mwaka wa fedha wa 2021/22.

Alisema kuwa tangu halmashauri hiyo ilipoanza utaratibu wa kukusanya mapato kwa mashine za kielekroniki na kuyapeleka benki, watendaji hao wamekuwa na tabia ya kutopeleka fedha hizo benki, badala yake wamekuwa wakitumia fedha mbichi kwa matumizi yao binafsi.

Misungwi alisema katika halmashauri hiyo, watendaji 93 wametumia Sh. 162,742,350 (milioni 162.7), hivyo kuwataka warudishe kabla ya Februari 28, vinginevyo ataliagiza Jeshi la Polisi kumkamata kila mtendaji anayedaiwa.

"Ninaagiza kuanzia leo (jana) hadi Februari 28, kila mmoja arudishe kiasi cha fedha anazodaiwa, ikipita tarehe hiyo nitampa orodha OCD inayoonyesha kila mtendaji kiasi anachodaiwa na kijiji alichopo na nitamwagiza amkamate ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake," alionya.

Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Daud Sichone, alisema baraza linaunga mkono agizo la Mkuu wa Wilaya huyo kwa kuwa halipo tayari kuona watendaji wa serikali wanaongoza kuhujumu kodi za wananchi.

## Uwezo wa kujieleza kupunguza unyanyasaji

**Na Christina Haule, DODOMA**

UWEZO wa wanawake kujieleza ndiyo njia pekee ya kuwasaidia kuondokana na vitendo vya ukatili wa aina zote wanavyofanyiwa na wanaume.

Hatua hiyo pia imeelezwa kusaidia kupunguza au kuondoa vitendo vya ukatili wa kingono mahali pa kazi.

Meneja Mikakati na Mipango kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Sylivia Dauli, alisema hayo jana wakati wa mdahalo wa masuala ya uwezeshaji wanawake na vijana chini ya mradi wa Vunja Ukimya uliofanyika jijini hapa.

Dauli alisema ule ukatili mkubwa sana wa kijinsia wanaotendewa wanawake wawapo kazini, lakini wanaweza wasiseme kutokana na kulinda ajira zao au kuogopa.

"Ifike mahali wanawake wenyewe wavunje ukimya, waseme wanayofanyiwa na hiyo itakuwa ndio njia sahihi ya kuwaondoa kwenye wimbi la ukatili wa kijinsia kwani serikali pia itafuatilia kwa makini na kukemea matendo hayo.

Wako wanawake ambao wanafikia hatua ya kuacha kuendelea na kazi au kuacha kuendelea na mafunzo ya vitendo kutokana na kukutana na vitendo hivyo tangu wawapo kwenye mafunzo ya awali, wanapata woga na kuacha, tasnia inaendа wapi," alisema.

Dauli pia alisema wakati umefika sasa kwa viongozi wa vyombo vya habari kuangalia kama kuna sera za kupinga masuala ya ukatili wa kijinsia kwenye vyombo vyao zinazozungumzia kuwalinda waandishi na masuala ya ukatili wa kijinsia kwa mapana na sio kuzingatia dhana za jinsia na usawa wa kijinsia mahali pa kazi pekee.

Sambamba na hilo, aliiomba serikali kupitia Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, kuangalia uwezekano wa kuzuia ukatili wa kijinsia ukiwamo wa kingono kwa wanawake na vijana kwenye vyombo vya habari.

# RC ataka maofisa TRA kujitathmini

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

MKUU wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, amewataka maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani hapa kuwajibika ili kuhakikisha makusanyo ya kodi na tozo yanaongezeka.

Gabriel alisema hayo jana wakati akifungua na kufunga mafunzo ya siku moja ya waandishi wa habari yaliyoandaliwa na mamlaka hiyo.

Alisema maofisa wa TRA hawana budi kuwajibika kila mmoja kwa nafasi yake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyabiashara na kusisitiza utoaji wa stakabadhi sahihi kwa wafanyabiashara pindi wanapowauzia wateja bidhaa.

Mkuu huyo wa mkoa alisema maofisa wa mamlaka hiyo wanapaswa kuwajibika kwa nafasi yake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyabiashara kila mara na kusisitiza utoaji wa stakabadhi sahihi kwa wafanyabiashara pindi wanapowauzia wateja.

Aliitaka TRA kutumia waandishi wa habari kuhamasisha ulipaji wa kodi za serikali kwa hiari sambamba na kutoa elimu kwa wafanyabiashara na jamii kwa ujumla.

"Tumieni waandishi wa habari kwa maana hili ni jeshi kubwa. Kutokana na kazi zao wana nafasi kubwa ya kukutana na makundi mbalimbali katika jamii wakiwamo wafanyabiashara," alisema.

Meneja wa TRA Mkoa wa Geita, Hashim Ngoda, akitoa taarifa ya makusanyo ya kodi na tozo mbalimbali, alikiri kufungwa biashara 660 kwa mwaka wa fedha 2019/20 kutokana na sababu mbalimbali.

Miongoni mwa sababu hizo ni wafanyabiashara kuhama maeneo ya kibiashara au kazi huku akibainisha kuwa pamoja na kufungwa, biashara mpya 1944 zimefunguliwa na kusajiliwa.

Biashara 660 zimefungwa mkoani hapa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo wafanyabiashara kuhama eneo hii kutokana na kupitia changamoto mbalimbali," alisema Ngoda.

Meneja huyo alisema mamlaka hiyo imekusudia kukusanya Sh. bilioni 31. 95 hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha unaotarajiwa kumalizika Juni 30, mwaka huu.

Pia alisema mamlaka hiyo imekusanya Sh. bilioni 15.23 kwa kipindi cha miezi sita kwa mwaka wa fedha Julai hadi Desemba, 2020, kupitia kodi na tozo mbalimbali, sawa na asilimia 97 ya malengo yaliyowekwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Geita (GPC), Renatus Masuguliko, aliipongeza TRA kwa kutoa mafunzo hayo, hivyo kuiomba kuweka utaratibu kuwajengea uwezo katika masuala ya kodi kila mara.




Meneja wa Kitengo cha Wateja Maalumu Benki ya CRDB, Crispin Sichalwe, akitoa mada katika Kikao Kazi cha Watendaji wa Kata na Mitaa ya Jiji la Dar es Salaam jana, kilichodhaminiwa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Bunge laitaka SIDO kubuni teknolojia ya kisasa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, imeliagiza Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kubuni utoaji wa huduma zinazotumia teknolojia ya kisasa ili kukuza viwanda vidogo na kuongeza ajira.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Erick Shigongo, alitoa agizo hilo jana jijini hapa katika semina iliyolenga kuwaelimisha wajumbe wa kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya SIDO na mafanikio yake.

Aliitaka SIDO kuongeza jitihada katika kufanya utafiti na ubunifu katika utengenezaji wa mitambo ya kisasa na inayokidhi mahitaji na kufanyia kazi mawazo ya vijana wengi ambao ni wabunifu, lakini hawana mitaji ya kuendeleza ubunifu wao.

Naye Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema serikali inaendelea kuiwezesha SIDO kuboresha mitambo yake kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kuzalisha mitambo yenye ubora unaokidhi mahitaji na soko shindani la mitambo kutoka nje ya nchi.

Alisema SIDO imeendelea kujenga mabanda katika kila mkoa kwa ajili ya wajasiriamali kuanzisha viwanda katika maeneo hayo kwa urahisi.

Pia alisema SIDO imejipanga kutanua uwigo wa utuoaji huduma inayopatikana katika mikoa yote na sasa kuelekeza huduma hizo katika kila wilaya ili kuongeza kasi ya uanzishaji na ukuzaji wa viwanda vidogo nchini ambavyo vitaongeza ajira na kukuza biashara na uchumi wa nchi.

Akitoa mada kwa wajumbe wa kamati hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Mhandisi Prof. Sylvester Mpanduji, alisema SIDO inatoa huduma za kiufundi na maendeleo ya teknolojia na viwanda hususani teknolojia za kuchakata mazao ya kimkakati kama korosho, alizeti, chikichi na nafaka katika vituo saba vya kuzalisha teknolojia kwenye mikoa ya Lindi, Mbeya, Iringa, Arusha, Moshi, Shinyanga na Kigoma.

Alisema huduma nyingine inayotolewa na SIDO ni kuendeleza ubunifu wa teknolojia kwa kutumia programu ya kiatamizi inayowalea, kuwapa mafunzo, kuwapa nafasi ya kufanyia kazi ndani ya eneo la shirika bure na kuwaunganisha na taasisi za kifedha wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kuhusu mafanikio ya SIDO kati ya mwaka 2016/17 - 2019/20, mkurugenzi mkuu alisema imeanzisha viwanda vidogo 4,410, viwanda vidogo 3,406 na viwanda vya kati 460.

Pia alitaja baadhi ya viwanda vikubwa vilivyoanzia SIDO kuwa ni pamoja na Dabaga kilichoko mkoani Iringa, Mwanza Quality Wine cha Mwanza, Tausi Coffee kilichoko Shinyanga na Mart Super Brand kilichoko Manyara.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kocha mpya Taifa Stars asiletwe kwa majaribio

**M**ABOSI wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wametangaza rasmi kuvunja mkataba na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, ambaye ni raia wa Burundi.

Uamuzi huo ulitangazwa na shirikisho hilo linaloongozwa na Rais, Wallace Karia ambaye ameingia katika mwaka wake wa mwisho wa uongozi, kabla ya uchaguzi mwingine utakaofanyika baadaye mwaka huu bila kuweka wazi sababu zilizopelekea kufikia uamuzi huo.

TFF imefanya uamuzi huo ikiwa ni siku chache baada ya Ndayiragije, Kocha wa zamani wa klabu za Mbao FC, KMC FC na Azam FC, kushindwa kuivusha Taifa Stars kwenye hatua ya makundi katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo Taifa Stars ilikuwa inashiriki huko nchini Cameroon.

Shirikisho hilo limesema litatangaza mrithi wa mikoba ya Ndayiragije baada ya kukamilisha mazungumzo na mchakato wa kupata kocha huyo mpya hivi karibuni.

Ndayiragije mbali na kuipeleka Taifa Stars katika fainali za CHAN mwaka huu, lakini pia ameipeleka hatua ya makundi timu hiyo kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia.

Kwa maana hiyo, kocha mpya atakayekuja anatakiwa kuanzia hapo alipoishia Mrundi huyo na kubwa wadau wa soka wakihitaji kuona Tanzania inapeperusha vyema bendera ya nchi katika michezo hiyo.

Tunapenda kuikumbusha TFF pamoja na Idara ya Ufundi kuwa kocha mpya itakayemleta awe ni mwenye kuendeleza programu zilizopo na si kuanza upya kwa sababu atatufanya turudi nyuma kwenye safari yetu ya mafanikio au katika kufikia 'ndoto' za kushiriki michuano hiyo ya juu duniani.

TFF inatakiwa kuajiri kocha ambaye ana uzoefu na mazingira ya Afrika na aliye tayari kufanya kazi kwenye timu za vijana kama ilivyokuwa kwa Ndayiragije kwa sababu taifa letu bado halina wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa kama zilivyo nchi zilizoendelea.

Inafahamika Taifa Stars inategemea wachezaji wengi zaidi kutoka kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo kocha mpya atakayeajiriwa asiwe 'mchoyo' wa kutoa mawazo kwa makocha wanaofundisha katika ligi hiyo ili pale atakapowaita wachezaji kwenye kambi yake asianze kutoa mafunzo ya awali na badala yake aendelee na programu kulingana na jukumu lililoko mbele yake.

Kocha huyo mpya aletwe kwa ajili ya kuinyanyua Tanzania hapa ilipo na kuisogeza mbele na asije kwa ajili ya kuvuna au kuweka mbele maslahi yake binafsi.


Tunatarajia kuona mabosi wa TFF wanaingia mkataba na kocha ambaye hatakuwa wa majaribio kwa sababu Taifa Stars inahitaji kufanya vyema katika mashindano yote itakayoshiriki na mawazo ya kuajiri kocha wa majaribio yasipewe nafasi.

Kama majirani zetu wa Ukanda wa Afrika Mashariki, Uganda na kikosi chao cha Uganda Cranes wanapata nafasi ya kushiriki katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwa vipindi viwili vinavyofuatana, basi hata Taifa Stars inaweza kufuzu tena katika fainali zinazofuata endapo uamuzi sahihi wa kuajiri kocha utafanyika.

Katika mchezo wa soka hakuna miujiza, benchi imara, wachezaji kujituma na maandalizi yanayostahili ndio vitu pekee ambavyo vitaipatia Taifa Stars matokeo chanya katika mashindano yote itakayokwenda kushiriki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Ndugu chungu jirani mkungu

**NDUGU** huwa kama chungu lakini jirani ni kama kifuniko cha chungu. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa ndugu huwa na uhusiano wa karibu sana kuliko mtu na jirani yake.

Kutoka makao makuu ya Klabu ya Simba pale Msimbazi mpaka yalipo makao makuu ya Yanga kule Jangwani ni mwendo wa kumtoa mtu jasho lakini timu hizo ni ndugu kwa sababu zinatoka katika ardhi moja ya Tanzania, zilizo kwenye jiji moja liitwalo Dar es Salaam ambalo zamani liliitwa Bandari ya Salama.

Yanga na Simba ni timu za Tanzania zinazotambulika zaidi Afrika kwani ndizo zilizoanzishwa mwaka 1935 lakini mwaka 1936 zikafarakana ilipoundwa Sunderland ambayo sasa yaitwa Simba. Timu hizo ziko radhi kufungwa mabao mengi na timu zingine kuliko kufungwa bao moja tu zinapopambana zenyewe!

Zamani timu hizo ziliposhindana hakukuwa na ugomvi baina ya wanachama au mashabiki wao kama ilivyo sasa.

Nakumbuka jinsi watu wawili wa vilabu hivyo walivyochemsha 'dawa' zao kwenye vyungu pale kwenye makutano ya barabara za Mafia na Msimbazi na wakiwa wamekaribiana kabisa huku wanachama na mashabiki wa pande zote mbili wakipita na kutumbukiza hela kwenye sahani ya kila upande huku bendera za timu zote zikipepea.

Kama hiyo haitoshi, timu moja kati ya hizo iliposhinda nyingine na kutwaa kombe, watu wanaoeleweka klabuni walilitembeza jiji zima na walipofika makao makuu ya timu iliyoshindwa walisimama na kulionyesha kombe hilo kwa watani zao.

Bila kupepesa macho, walioshindwa walitumbukiza kiasi fulani cha pesa ndani ya kombe kuwapongeza washindi. Mambo hayo hayapo siku hizi kwani hakuna upande unaothubutu kufanya hivyo, kwani wanaepusha taharuki, yaani hali ya kuwa na wasiwasi kuhusu matokeo yatakayofuata.

Enzi zile, hata mashabiki wa timu zote walikuwa wakienda uwanjani pale Karume jijini pamoja na kushangilia timu zao zinapofunga na kuzunguka uwanjani bila kufanyiwa bughudha yoyote.

Hakuna utani huo siku hizi kwani upande wowote utakaofanya hivyo utajuta kwa mambo watakayofanyiwa na wenzao wa upande mwingine! Ujinga mtupu!

Yanga na Simba zapaswa kutambua kuwa 'Nahodha hodari haogopi mawimbi' Maana yake nahodha stadi hayaogopi mawimbi ya bahari. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano shujaa ambaye hatishiwi au kutiwa woga na jambo fulani. Shujaa huwa tayari kupambana na hali yoyote ile itokeayo.

Wahenga walisema: "Hasama (uadui) ndimi za moto" wakiwa na maana uadui au adawa ni kama ndimi za moto ambazo huchoma. Methali hii yatuhimiza tujiepushe na uadui unaoweza kutuletea maangamizo makubwa.

Hivi karibuni msemaji wa Simba alipendekeza wana Yanga wasiruhusiwe kuingia uwanjani timu yake itakapopambana na timu ya ughaibuni kwani timu hiyo ngeni ingeshangiliwa sana na mashabiki wa Yanga! Wazo hilo halikukubaliwa.

Siku ilipofika, ni kweli kulikuwa na baadhi ya mashabiki wachache wa Yanga waliohudhuria ili kuishangilia timu ngeni! Hata hivyo wageni walifungwa mabao 4-1 na kuwatuliza wale waliokuwa wakishangilia timu ngeni!

Mashabiki wa Yanga wakatulia tuli (bila ya kutikisika) kama maji mtungini na kuondoka uwanjani kabla ya mchezo kumalizika! Aibu iliyoje!

Ni kweli kuwa wachezaji wa timu ngeni walifurahi waliposhangiliwa na baadhi ya wenyeji, yaani wale jamaa wa Yanga waliokuwa wakishangilia kabla ya kufungwa, lakini pia walishangazwa walipoona timu yao ikishangiliwa na wenyeji waliovaa jezi za Yanga!

Niliwauliza baadhi ya wana Yanga wenzangu waliokuja nyumbani lakini sikukubaliana na majibu yao hasa mmoja wao aliponijibu kwa Kiingereza: "Tit for tat" akimaanisha "jicho kwa jicho." Badala ya kumjibu moja kwa moja, kutokubaliana naye nikavuta Biblia yangu na kumsomea ifuatavyo:

"Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote. Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote. (Warumi 12:9,14-18).

"Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, maana imeandikwa: 'kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa;' anena Bwana. "Lakini, adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe; maana ufanyapo hivyo; utampalia makaa ya moto kichwani pake.

"Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa neema." (Warumi 12:19-21).

**marobarnabas@yahoo.com 0784334096**

# Bilioni 33/- kujenga hospitali za wilaya

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema katika mwaka wa fedha 2020/21, serikali imetenga Sh. bilioni 33.5 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali 67 za halmashauri.

Naibu Waziri, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Busega (CCM), Simon Lusebgekile, aliyetaka kujua lini serikali itapeleka vifaa katika Hospitali ya Wilaya ya Busega ili huduma bora za afya ziendelee kutolewa.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya hospitali hiyo ili kuendelea na ujenzi.

Alisema kwa mwaka huu, serikali imetenga Sh. bilioni 33.5 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali hizo 67 ikiwamo ya Busega.

"Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega ni miongoni mwa hospitali 67 za halmashauri zilizoanza kujengwa mwaka 2018/19 kwa kupewa fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba ambayo ni: Jengo la utawala; Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD); Jengo la Maabara; Jengo la Mionzi; Jengo la wazazi; Jengo la Kufulia; na Jengo la Kuhifadhia Dawa," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alihoji ni lini serikali itapeleka watumishi wa afya wa kutosha na vifaa tiba kwenye Hospitali ya Wilaya Nkasi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dugange alisema uboreshaji wa miundombinu na upatikanaji wa watumishi ni kipaumbele cha serikali na imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili hiyo ili kuwe na huduma bora kwa wananchi.

# Mbunge alia mgogoro wa hifadhi na wananchi




Habari na Augusta Njoji

MBUNGE wa Kwela (CCM), Deus Sangu, ameitaka serikali kutatua mgogoro wa ardhi katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Pori la Akiba Uwanda mkoani Rukwa kutokana na askari wanyamapori kuwanyang'anya wananchi mali zao.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema katika oparesheni za askari wanyamapori, kumekuwa na tabia ya askari kunyang'anya wananchi mali ikiwamo boti na mali zingine.

"Ninataka kujua kauli ya serikali, ni nini kwa sababu askari hao wakikamata mali hizo na kuwa nazo zaidi ya miaka miwili au mitatu ambayo ni hasara pia kwa serikali na wananchi kuwa maskini?

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema masuala ya kisheria yanapokuwa chini ya mahakama, wahifadhi hutegemea uamuzi wa mahakama.

"Lakini pia ushahidi tunabaki nao ikiwamo vitu alivyokamatwa navyo. Wizara ipo tayari kuangalia migogoro iliyopo kwenye eneo hilo na tutasuluhisha kadri inavyowezekana," alisema.

Masanja alisema Pori la Akiba Uwanda lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5,000, lilianzishwa mwaka 1959 na kutangazwa upya kwa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 12 ya Mwaka 1974, kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la Novemba 8, 1974.

Alisema kuwa tangu mwaka 1974 hadi 2013, pori hilo lilikuwa likisimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na lilikabidhiwa rasmi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii Januari 20, 2014.

"Pori hilo linapakana na vijiji 11 vya Ilambo, Kilyamatundu, Mkusi, Kapenta, Maleza, Kilangawana, Mpande, Legeza, Nankanga C, Liwelyamvula na Kipeta na vijiji saba vya Maleza, Kilangawana, Mpande, Legeza, Nankanga C, Liwelyamvula na Kipeta ndivyo vyenye mgogoro na Pori la Akiba Uwanda," alisema.

Naibu waziri huyo alisema kutokana na mgogoro huo, orodha ya vijiji husika iliwasilishwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Migogoro iliyojumuisha wizara nane na utekelezaji wa ripoti ya utatuzi wa migogoro ya ardhi ya mawaziri hao chini ya uenyekiti wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ndiyo utaleta ufumbuzi wa mgogoro huo na mingine iliyopo.

"Tunaomba Mheshimiwa Deus pamoja na Watanzania wote, tuwe na subira wakati utekelezaji wa ufumbuzi unaratibiwa," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mbunge wa Same Magharibi, Dk. David Mathayo David Bungeni, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# REA awamu ya tatu kuanza mwezi huu

WIZARA ya Nishati imeliarifu Bunge kuwa mradi wa upelekaji umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili, unatarajiwa kuanza mwezi huu na utakamilika Septemba 2022.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme wa REA kwenye baadhi ya vitongoji vya vijiji vya Namtumbo.

Akijibu swali hilo, Byabato alisema serikali kupitia Shirika la Umeme (TANESCO) pamoja na REA, inaendelea kupeleka umeme katika vijiji na vitongoji nchini.

"Vijiji vyote vilivyobaki katika Wilaya ya Namtumnbo, vitapatiwa umeme kupitia mradi huu, utahusisha pia kupelekea umeme vitongoji vya vijiji vitakavyopelekewa umeme," alisema.

Aliwahakikishia wabunge kuwa vitongoji vyote nchini vikiwamo vya Wilaya ya Namtumbo, vitaendelea kupelekewa umeme kupitia miradi ya umeme vijijini kulingana na upatikanaji wa fedha.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo aliitaka serikali kuagiza uharakishaji wa kuunganishiwa umeme wananchi ambao wameshakidhi vigezo lakini hadi sasa hawajaunganishiwa huduma hiyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Byabato alisema wilaya hiyo ilikuwa miongoni mwa wilaya zilizopaswa kupata huduma hiyo katika mzunguko wa kwanza na baada ya kufanyika kazi ya awali, wakandarasi wengi waliongezewa kazi za nyongeza ili kufikia wananchi.

"Namtumbo ni wilaya ambayo iliongezewa kazi ya nyongeza na kusababisha kushindwa kukamilika kwa wakati na hivyo mkandarasi aliyekuwa anafanya kazi Mkoa wa Ruvuma, anatarajiwa kukamilisha kazi kwenye mkoa huo Aprili mwaka huu.

"Kilichobaki ni upelekaji wa mita ili kuwaunganishia huduma wananchi na ifikapo Aprili, watakuwa wameunganishiwa," alisema.

# Shule yapewa tuzo kuongoza miaka sita

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St. Anne Marie Academy imepewa ngao kutambua mchango wake kwenye sekta ya elimu kwa kuendelea kufanya vizuri kitaaluma kwenye matokeo ya kitaifa shule yake ya msingi na sekondari.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo zilizoandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilifanyika hivi karibuni na Ofisa Elimu Msingi Manispaa ya Ubungo, Abdul Buhety, alikabidhi tuzo mbalimbali kwa shule zilizofanya vizuri kwenye mtihani wa darasa la saba mwaka 2019/20.

Ofisa huyo aliipongeza shule hiyo iliyoko Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam kwa kuwa ya kwanza Mkoa wa Dar es Salaam na ya nane kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana.

Alisema shule hiyo imeongoza Mkoa wa Dar es Salaam miaka sita mfululizo na iliingia 10 bora kitaifa ikiwa shule pekee yenye wanafunzi zaidi ya 100 ambao wote walifaulu kwa daraja A.

Baada ya kupokea ngao hiyo, Mkuu wa Shule hiyo, Gladius Ndyetabula alisema mafanikio hayo ni matunda ya ushirikiano baina ya uongozi wa shule, walimu na watumishi wote.

Alisema imekuwa kawaida kwa shule hiyo kuwapa motisha wanafunzi wa shule hizo kila wanapofanya vizuri kitaaluma na ndiyo sababu shule imekuwa ikipata matokeo mazuri kwenye mitihani mbalimbali ya kitaifa.

Ndyetabula alisema wanatarajia kuanza kuwapeleka nchini Dubai, Uingereza hadi Marekani wanafunzi watakaokuwa wanafanya vizuri kwenye mitihani yao, ili iwe chachu kwa wengine kufanya vyema kwenye mitihani ya ndani na ile ya kitaifa.

"Shule imejiwekea utaratibu wa kuwapa motisha wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi na huwa tunakawaida ya kuwapeleka mbuga za wanyama kama Serengeti, Mikumi, Ngorongoro hivyo tutaanza kuwapeleka ulaya," alisema.

Juni mwaka 2019, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwamwagia sifa wanafunzi wa Shule ya St. Anne Marie Academy kwa kufanikiwa kuwa wa kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2018.

# Serikali yaanzisha tiba mtandao

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), imeanzisha mradi wa tiba mtandao ambao utamwezesha bapo daktari bingwa kumhudumia mgonjwa aliyeko pembezoni kwa njia ya mtandao.

Waziri Dk. Faustine Ndugulile aliyasema hayo jana katika kikao cha wizara hiyo na Kamati ya Bunge ya Miundombinu ambacho kilikuwa kikipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya UCSAF.

Alisema kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), madaktari wa kibingwa watatoa huduma kwa njia hiyo.

"Kusudio letu ni sekta hii iwe ni njia kuu za uchumi kama ilivyo barabara. Huko tunakoenda kupitia mkongo sekta hii itakuwa moja ya zinazotengeneza uchumi na majukumu yetu ndani ya miaka mitano kuhakikisha tunafikisha mkongo wa taifa kwa asilimia 85," alisema.

Alisema wizara hiyo inatengeneza mazingira wezeshi juu ya matumizi ya TEHAMA, ndani ya serikali ili taasisi za serikali ziwasiliane kwa njia za mawasiliano.

Pia alisema kwa sasa nchi imeingia uchumi wa kati, hivyo inapaswa kuendana na dunia kuhusu uchumi wa kidijitali biashara mtandao na mapinduzi ya viwanda.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Moshi Kakoso, alisema wabunge watahakikisha wanashirikiana na serikali kuhakikisha mfuko huo unaimarika na kufikia malengo yake.

Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, alipongeza mfuko huo kwa kupeleka elimu shuleni kuhusiana na TEHAMA, hivyo kurahisisha mawasiliano. Alishauri makandarasi wanaopewa kazi ya kujenga minara kukamilisha kazi hiyo kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano.

Awali, akiwasilisha mada katika semina hiyo, Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashaba, alisema mradi wa tiba kwa mtandao upo katika hatua za awali.

"Kwa kuanzia tunatengeneza mtandao ambapo daktari aliyopo kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wale wataalamu bingwa, kwa mfano unamtafuta Prof. Janabi mtaalamu wa moyo, kuna Mtanzania yupo Kigoma anahitaji huduma sio lazima kusafiri kufuata huduma za moyo tunataka kuunganisha kupitia mtandao," alisema.

Pia alisema mfuko huo umekuwa ukitekeleza miradi mbalimbali ikiwamo upelekaji mawasiliano vijijini kupeleka vifaa vya mawasiliano kwenye shule za umma.




Meneja wa Bidhaa za Tigo, Mkumbo Muyonga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa simu za Samsung Galaxy 21, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MIHB yabainisha mikakati kuhusu bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Mico Halal International Bureau (MIHB), imeweka wazi mipango ya shughuli zake huku ikiomba kuwa mwanachama wa Shirika la Hafsa la Uturuki linalosimamia bodi za Halal duniani.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa MIHB, Sheikh Jumanne Kasonso, wakati akizungumza kuhusu kuanza kazi kwa taasisi hiyo nchini.

Alisema Hafsa ni Bodi ya Uturuki ambayo huzileta pamoja taasisi za Halal duniani kote.

Kasonso alisema lengo kuu la Hafsa yenye makao yake makuu kwenye mji wa Istanbul Uturuki ni kuweka viwango sawa vya Halal kwa ajili ya kutumiwa na taasisi za Halal kote duniani.

Mbali na kuomba uanachama wa Hafsa, alisema MIHB pia imeomba bodi inayosimamia Halal nchini Malaysia ili itambulike kama taasisi ya kimataifa inayosimamia Halal nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa Sheikh Kasonso, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) limeipa mamlaka MIHB kusimamia uchinjaji wa wanyama kwenye machinjio yote nchini.

Alisema MIHB inajihusisha na kutoa vyeti vya Halal katika machinjio, bucha, migahawa, majiko na kwenye shughuli za mapishi. Na kwamba wanafanya ukaguzi na uchambuzi inapobidi na kuhamasisha bidhaa za Halal kupitia vyombo vya habari vya kielektroniki na magazeti.

Lengo kuu, alisema ni kuondoa kabisa wasiwasi wa bidhaa hizo za Halal kwa watumiaji wake kwa kuendelea kufanya ukaguzi kuanzia sehemu inapopatikana bidhaa hiyo kwenda kwa mtumiaji wa mwisho kuhakikisha mtumiaji anatumia bidhaa iliyo halal.

Sheikh Kasonso alisema jukumu lao kuu lingine ni kuhakikisha vigezo vyote vinafuatwa kwa bidhaa hizo kukubalika kimataifa na kutambuliwa kutokana na kukidhi vigezo.

"Kuhusu usafi kwa watumishi watakaohusika na kuhudumia vyakula kwa kila eneo lazima wawe wamepimwa kabla ya kupata hiyo kazi na afya yao kufuatiliwa kwa karibu kwa muda wote wa ajira yao," alisema.

## Gwajima ataka wakiukaji maadili wachukuliwe hatua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza mabaraza na vyama vya kitaaluma kuchukua hatua dhidi ya watumishi wanaokwenda kinyume cha maadili ya taaluma zao.

Dk. Gwajima, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano wa wauguzi viongozi.

"Jukumu letu kama viongozi ni kusimamia watumishi walioko chini yetu ili watoe huduma kwa wateja kwa kuzingatia maadili katika utumishi wa umma na kuepukana na matendo mabaya. Niagize mabaraza na vyama vya kitaaluma kuendelea kukemea na kuchukua hatua dhidi ya watumishi wanaokwenda kinyume na maadili ya taaluma yao," alisema Dk. Gwajima.

Pia alisema suala la maadili linatakiwa kupewa kipaumbele ili kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi kwani hivi sasa kumekuwa na kuporomoka kwa maadili ya watumishi katika sekta ya afya.

"Tunapaswa kujiuliza maadili ya mtumishi wa umma awe kiongozi au mtumishi wa kawaida ni nini? Maadili inafafanuliwa kwamba ni matendo mema, kwa hiyo maadili ni viwango vya uadilifu vinavyotazamiwa na wananchi kwa mtumishi yeyote wa umma, maadili huwekwa kwa njia ya misingi, kanuni na miongozo inayotakiwa katika utumishi," alisema.

Aidha, alisema mara nyingi wanapokea malalamiko juu ya ucheleweshaji wa utoaji huduma, upendeleo, mienendo mibaya ya watumishi, ubinafsi katika kazi rushwa, vitendo vya jinai (wizi) na matuumizi mabaya ya madaraka.

Alisema wauguzi na wakunga ni raslimali kubwa na nguvu kubwa katika sekta ya afya nchini.

"Ni watoa huduma ya afya ambao wako mstari wa mbele katika kutoa huduma wakati wote kwa kuwahudumia wagonjwa wenye uhitaji wakati wote, hufanya kazi saa 24 siku saba kwa wiki wakitoa huduma za afya kwa zaidi ya asilimia 80 ya huduma zote za afya," alisema.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitenga mwaka 2020 kuwa wa wauguzi na wakunga duniani na kuadhimishwa katika nchi mbalimbali kama kuenzi mchango muhimu unaotolewa na wauguzi na wakunga katika kuleta mapinduzi makubwa katika huduma ya afya.

# Waziri TAMISEMI ageukia bima ya afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Festo Dugange, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF), ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya.

Dk. Dugange aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizindua ugawaji wa kadi za iCHF kwa watoto 361,539 wanaoishi katika mazingira hatarishi kwenye mikoa 24 nchini.

Aliwashukuru wadau waliowezesha upatikanaji wa bima hizo za afya ya jamii kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuwataka kazi hiyo kuwa endelevu ili watoto hao wawe salama wakati wote.

"Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) kwa msaada mkubwa wanaotoa kwa serikali kuwahudumia watoto walio katika mazingira hatarishi kupitia miradi mbalimbali ukiwamo huu wa USAID Kizazi Kipya unaotekelezwa na Shirika la Pact Tanzania ambao umefanikisha upatikanaji wa bima hizi za afya ya jamii," alisema Dk. Dugange.

Alisema mradi huo wa USAID Kizazi Kipya katika kipindi chake cha miaka mine, umekuwa na manufaa makubwa kwa watoto wetu walio katika mazingira hatarishi zaidi ya 70,000 wamenufaika kwa kupata vifaa vya shule, mafunzo ya ufundi, vifaa vya kuanzia biashara na huduma za afya na VVU/UKIMWI.

"Upatikanaji wa bima za afya kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kaya zao ni msaada wenye tija kwetu kwa kuwa sasa familia hizo zina uhakika wa kupata huduma za afya katika kipindi chote cha mwaka bila kuwa na wasiwasi wowote," alisisitiza.

Aliwataka wataalamu wa afya nchini kote kuhakikisha kuwa familia zilizopatiwa kadi za bima ya afya ya jamii na wananchi wote kwa ujumla walio katika mfumo wa bima hii wanapata huduma za afya bila shida yoyote.

"Sasa CHF iliyoboreshwa iwe agenda ya kudumu katika vikao vyote vya kiutawala katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuleta mwamko kwa wananchi wote kujiunga na mfuko huu waweze kunufaika na kitita cha mafao kinachopatikana kupitia CHF," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Afya Ustawi wa Jamii na Lishe, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema msaada huo umegharimu Sh. bilioni 4.6 kutoka Pact-Tanzania.

"Fedha hizo mbali na kunufaisha watoto waliokatika mazingira hatarishi na kaya zao kwa kupata huduma za afya mwaka mzima na pia zitawezesha vituo kuboresha huduma za afya ikiwamo kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba," alisema Dk. Ntuli.




Makamu Mkuu wa Shule ya St. Anne Marie Academy, Amos Joseph (katikati) na wanafunzi wa shule hiyo, wakifurahia ngao ya ushindi shuleni hapo jana, iliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia baada ya shule hiyo, kuongoza kwa miaka sita mfululizo kwenye matokeo ya kitaifa ya shule ya msingi katika Mkoa wa Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yataka taarifa za rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, imesema itaendelea kutoa elimu ya kupiga vita rushwa, huku ikiwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa zenye viashiria vya rushwa ili zifanyiwe uchunguzi.

Akizungumza na gazeti hili Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, taasisi hiyo itaendelea na utoaji elimu kwa wakazi wa jijini Dodoma kupitia mikutano ya hadhara, lakini watashirikiana na klabu za kupinga vitendo dhidi ya rushwa zilizoko jijini hapa kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya suala la rushwa.

Kibwengo alisema taasisi hiyo imepanga muda wa kutembelea katika maeneo mbalimbali jijini hapa, kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi ya namna ya kupinga rushwa katika maeneo wanayoishi ikiwamo sehemu za kazi.

"Elimu inayotolewa inasaidia sana kwa sababu wananchi wanaonekana kuelewa, kutokana na namna wanavyowasilisha baadhi ya taarifa katika ofisi zetu," alisema Kibwengo.

Pia aliitaka jamii kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU wa kutoa taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa na kwamba taasisi itazifanyia uchunguzi wa kina ili kubaini kama zinaviashiria vya rushwa ndani yake ambapo hatua stahiki zitafuatwa. Kibwengo alisema mapambano dhidi ya rushwa ni ya kila mmoja, hivyo wananchi wanapaswa kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona sehemu kuna vitendo vya rushwa ambavyo vinamnyima mtu kufanya kazi kwa haki.

"Mwaka huu tumejipanga kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kupambana na rushwa, tutakuwa tukitumia mikutano na maonyesho ya hadhara kwa jamii ili waweze kupata elimu," alisema Kibwengo.

Akizungumzia kuhusiana na Klabu za Kupinga vitendo vya rushwa jijini hapa alisema zinaendelea kufanya vizuri katika maeneo hayo huku akiendelea kusisitiza taasisi hiyo itazidi kuziboresha ili zisaidie kuelimisha jamii.

Alisema, wameanzisha klabu hizo katika shule za msingi,sekondari pamoja na vyuo ambapo alisea TAKUKURU imekuwa ikizipitia mara kwa mara ili kuona namna gani zinashirikiana na walimu katika utoaji elimu dhidi ya kupiga vita vitendo vya rushwa.

"Klabu hizi zinasaidia sana kuwaelimisha wenzao kuhusu kupiga vita rushwa, kwa sababu wao tayari wamepata elimu hiyo kutoka TAKUKURU," alisema Kibwengo.



# SMZ yaandaa kongamano la uvuvi bahari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inakusudia kuanza kongamano kubwa litakalowakutanisha wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini yakiwamo majongoo.

Waziri wa Wizara hiyo, Abdallah Hussein Kombo, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa za maandalizi ya kongamano hilo litakalowakutanisha wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini.

Alisema wizara imejipanga kuhakikisha wananchi, wakiwamo wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini, wanatumia vizuri sana matunda na faida ya rasilimali ya baharini kwa ajili ya kibiashara.

Akizungumza jana na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar, alisema wananchi wakiwamo wavuvi bado hawajatumia vizuri uchumi wa buluu kwa kuvuna rasilimali zinazopatikana katika eneo hilo.

Waziri Abdallah alisema ufugaji wa mazao ya bahari, hasa majongoo ya pwani, ni moja ya maeneo ambayo yanaweza kuwakomboa wananchi kiuchumi.

Alisema soko la majongoo ya pwani katika nchi za Ulaya na Asia ni kubwa na la uhakika ambalo bado wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini hawajalitumia kwa kiasi kikubwa.

Pia waziri huyo alisema, serikali inatarajia kujenga chuo kikuu cha uvuvi na ubaharia ili wavuvi kupata taaluma.

Kuhusu kuchelewa kwa ujenzi wa soko la uvuvi la Malindi mjini Unguja, alisema hali hiyo imetokana na janga la corona.

Alisema makandarasi wa jengo hilo ni kutoka Korea, hivyo kwa sasa wamesita kuja kutokana na nchi kukabiliwa na janga hilo.

# Mwakilishi aibua matatizo huduma za afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Baraza la Wawakilishi (Viti Maalum), Mwanaidi Kassim, amesema licha ya serikali kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja bado kuna matatizo kwa baadhi ya huduma.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia hotuba ya Rais wa Zanzibar aliyoitoa wakati akifungua Baraza la Wawakilishi Novemba, mwaka jana.

Mwanaidi alisema baadhi ya huduma muhimu hazipatikani hospitalini hapo ikiwamo kipimo cha kupimia damu kwa watoto wachanga hali ambayo imesababisha usumbufu kwa wananchi.

Alisema watoto wanapotakiwa kufanyiwa kipimo hicho, wazazi hulazimika kuwapeleka katika hospitali binafsi ambako ni gharama na baadhi ya wananchi uwezo wao wa kifedha ni mdogo.

Kipimo hicho, alisema gharama yake ni Sh. 20,000 na watoto wanaohitaji huduma hiyo ni njiti, hivyo aliomba serikali kuangalia umuhimu wa kupatikana kwa kifaa hicho hospitalini hapo.

Pia alisema bado kuna tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama mijini na vijijini, hivyo kuiomba serikali kuhakikisha huduma hiyo muhimu inapatikana.

Naye Mwakilishi Mgeni Hassan Juma alisema Zanzibar ina rasilimali za bahari nyingi, hivyo ni vyema kuzitumia kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mgeni ambaye ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, alisema Zanzibar inaitumia bahari na fukwe kwa shughuli za utalii, uvuvi wa kawaida na uvuvi wa bahari kuu kwa shughuli ya gesi na mafuta, hivyo uchumi wa buluu ni fursa kubwa sana kuitumia katika masuala ya kiuchumi.

Alisema iko haja ya kusaidiwa wavuvi ili kuongeza kipato chao katika shughuli za uvuvi na kutaka kuwapo kwa vifaa na elimu ya kutosha kwa vyuo vya ufundi ili vijana wakimaliza masomo katika vyuo hivyo kuwa na ujuzi mzuri.




Waziri wa Vijana, Habari, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Mwita (kushoto) na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili, Soud Nahoda wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wataka elimu kuhusu uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Wanaume wa Mabadiliko kutoka Unguja, imeshauri kutolewa elimu kuanzia ngazi za chini kwa wanafunzi shuleni, mabaraza ya vijana na maeneo mengine ili kuwahamasisha vijana kushika nafasi mbalimbali za uongozi kupitia maeneo hayo.

Wanaume hao walisema hayo walipokuwa katika kikao cha pamoja kati yao na viongozi wa dini na watendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar kilichofanyika Kikwajuni, Unguja.

Walisema hatua hiyo itawasaidia vijana hao kuwa na uthubutu, utayari na kujiamini katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wanapofikia umri wa kufanya hivyo.

Asilimia kubwa ya wanawake, walisema wanashindwa kugombea nafasi hizo kutokana na kukosa msingi imara toka awali, hivyo kupitia maeneo hayo yatakuwa chachu ya kuwapika na kuwapata viongozi bora na wenye uwezo mkubwa hapo baadaye.

Katibu wa Kamati hiyo, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Hassan Jani, alisema mikakati zaidi inahitajika katika kuwahamasisha na kuwasaidia wanawake kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema licha ya juhudi kubwa zinazoendelea kuchukuliwa na taasisi hiyo na zingine katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa ili kufikia ngazi za uamuzi na uongozi bado jitihada zaidi zinahitajika.

Naye Mjumbe wa Kamati hiyo, Said Mtaji Askari, kutoka Wilaya ya Kati Unguja, alisema umefika wakati kwa jamii kuwaunga mkono wanawake na utafiti unaonyesha baadhi yao wanaoshika nafasi za uongozi, wana uwezo mkubwa wa kusimamia vyema dhamana zao na kuziletea mafanikio makubwa.

Ofisa Ufuatiliaji wa Miradi na Tathmini kutoka TAMWA, Mohammed Khatib Mohammed, alisema katika kufanikisha suala hilo, TAMWA imekuwa ikisimamia mradi wa kuwajengea uwezo wanawake kisiasa na kidemokrasia kwa lengo la kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uwongozi pale muda unapofikia.

Mradi huo wa miaka minne unaotekelezwa na TAMWA Zanzibar chini ya ufadhili wa UN Woman unalenga kuangalia ngazi za chini za uongozi ili kuwajengea uwezo wanawake kujiamini katika kugombea nafasi za uongozi.



**NANDY AJIFARIJI KUTUMIA MIL. 70** Uk.13

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI FEBRUARI 13, 2021



## KASHINDWA!

# Wema amkimbia kidume hakina sukari

KUMEKUCHA! Ni vita nyingine imeanza inayomuhusu mwigizaji mkongwe wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, baada msanii huyo kukiri uhusiano wake na mwanamume aliyetarajia kufunga naye ndoa, ulivunjika kutokana na kuwa na tatizo la kukosa nguvu za kiume.

Kauli ya Wema imekuja siku chache baada ya aliyekuwa mpenzi wake, Patrick Christopher, kumtaja mrembo huyo kama mtu ambaye hana malengo ya baadae ya maisha yake na pia mpenda starehe.

Hata hivyo, bila kumtaja jina, Wema amedai hana sababu nyingine ya kuachana na mpenzi wake huyo, bali ni kutokana na kushindwa kumtimizia hitaji lake la tendo la ndoa.

Staa huyo akishea na mashabiki wake Insta Live, amesema ni jambo baya kwa mwanamke kushindwa kupata mahitaji yake hasa tendo la ndoa, na ndio sababu aliamua kumbwaga chini.

"Nilikuwa kwenye mahusiano na mwanamume ambaye kwenye interview zangu nilikuwa namtaja sana, moja kati ya vitu ambavyo tulifanya tukaachana ni yeye kukosa nguvu za kiume, ilikuwa mbaya sana kwangu kwa sababu kila mtu anamatamanio yake na ukiwa kwenye mapenzi kitachofanya mapenzi yenu yanoge ni tendo la ndoa" amesema Wema.

Awali, akizungumza na EATV, Christopher alisema alikuwa kwenye uhusiano na Wema kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini waliamua kuachana baada ya kuvuja kwa video zikiwaonesha wakiwa faragha.

"Tulikaa kwenye mahusiano karibia miaka mitatu, yupo tofauti ni wanawake wengine wanaojituma yeye haijui ya baadae, anaishi kwa kuangalia leo tu na mpenda starehe, tulifikia hatua ya kuachana kwa sababu alikuwa anaposti vitu vya ajabu wakati mimi nina mtoto mkubwa na vilinileteа aibu kwenye jamii" amesema Christophe.

BASI SAWA

## Charz Baba wenzio walisema lakini...

MARA baada ya kuvunjika kwa ndoa yake ya pili, mkali wa muziki wa Dansi nchini, Charz Baba amesema amewaepuka wanawake kwani anahisi wanamchezea na kumtenda kwenye mapenzi.

Charz Baba amesema bado anajiona ni kijana na hapendi mambo ya kihuni ndiyo maana ameweza kutulia mwaka mmoja bila ya kukutana na mwanamke kimwili

"Mimi bado mvulana nina miaka 41, bado mdogo na sijakuwa, sasa hivi nina mwaka mmoja sijakutana na mwanamke kimwili, sitaki tena wanawake maana hawaridhiki naona wananichezea wananiacha sijui kwanini au labda nina kasoro gani, toka nianze kupambana kwenye ligi ya mapenzi napigwa mimi tu" ameeleza Charz Baba.



## Roma umeanza kuwakeraa

RAPA Roma Mkatoliki, ambaye kwa sasa anaishi Marekani, amewachana baadhi ya wasanii wa zamani akisema wanafanya vibaya pale wanapopewa nafasi jukwaani.

"Nianze na neno samahani kama nitawakwaza watu lakini pia ninaweza nikawa na maana, lengo langu sio kuwadharau ama kuwavunjia heshima wasanii wa zamani, baadhi yao wanatuangusha sana wanapopewa kipaza sauti na kupanda jukwaani kufanya shoo, mnachokitoa hakiendani na matarajio ya mashabiki"

Amesema kumekuwa na malalamiko nafasi wanazopewa na watu wengi hawatumii vizuri kutokana na kusahau nyimbo zao, badala yake muda mwingi wanatumia kwenye kusema mikono juu.





# Dogo Janja kalewa na mahaba

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Dogo Janja, amechanganyikiwa na penzi na sasa ameamua kuhama jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kwenda kumlinda mpenzi wake Quenlinna Totoo.

Dogo Janja ambaye kwa sasa anaonekana mara chache, amesema yuko Arusha na mchumba wake Quenlinna Totoo, na kwamba hajutii uamuzi wake huo.

"Dar Es Salaam nipo sana ila huwezi jua nilipo, nitatokea kukiwa na ishu muhimu maana sipendi kuonekana hovyo lakini watu wangu wa mtaani wanaiona kila siku, mapenzi hayajawahi kuniteka ila nayapenda na nikipenda huwa nipo karibu na mpenzi" amesema Dogo Janja



# Nandy ajifariji kutumia milioni 70

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Nandy, amejigamba kwamba wimbo wake mpya aliomshirikisha Koffi Olomide kutoka Congo DRC, umemgharimu zaidi ya shilingi Milioni 70.

Akizungumza na EATV, Nandy amesema hana wasiwasi na gharama za wimbo huo, hata kama usipompa faida yeye anachoamini ni kwamba atakuwa ameacha alama kwenye muziki wake.

"Sijaongeza sifuri mbele ila kwa mtu muelewa anajua ilivyo, kuna kurekodi video ambayo si chini ya Milioni 15 au 16, kumvalisha Koffi Olomide na watu wake, wachezaji, mimi mwenyewe, magari na hoteli zenye hadhi ya nyota tano zaidi ya Milioni 70, hata kama faida ikichelewa naamini itakuwa imeniachia alama" amesema Nandy.

# Uke wenza usikie tu

Na Adam Fungamwango

UKEWENZA ni kitendo cha mwanamke kuolewa na mwanaume aliye kwenye ndoa na mwanamke mwingine, iwe ya kidini, kiserikali, au ya kimila.

Lakini wanawake wengi hawapendi sana kukaa uke wenza kwa matatizo ambao wakati mwingine yanasababishwa na wao wenyewe.

Ni kwamba anayemtesa mwenzake na yeye akipata nafasi ya kumnyanyasa mwenzake, atafanya hivyo hivyo. Wenyewe wanakwambia uke wenza, afadhari umepate mwanamke wenzako kwenye huruma, lakini la sivyo utajuta.

Sababu ni kwamba kila mke anataka yeye aonekane bora zaidi kwa mume kuliko mwingine. Hapo ndipo zitatafutwa sababu za halali na zingine zizizo halali, ili mradi tu kila mmoja amvute mume.

Hapa ndipo baadhi yao wanaingia 'chimbo' na kuanza kufanyiana mambo ya kishirikina.

Lakini wanamuziki wa zamani wao hawana sehemu ambayo wamebakisha. Leo tunaziangalia nyimbo zilizozungumzia uke wenza.



KIDA WAZIRI

**Uke wenza-Marijani Rajab**

Ulitungwa na Marijani Rajab mwanzoni mwa miaka ya 1980, na kuuimba akiwa na bendi ya Dar International.

Hapa mwanamama mmoja anakutana na shoga yake, lakini kwanza anamsahau kwa jinsi alivyopururuka.

Anamuuliza jinsi ya kuchuja urembo wake, mwenzake anamwambia ni kwa sababu ya ukwe wenza.

Anamkumbusha kuwa uke wenza ni fahari ya kinababa, lakini kwao wanawake ni matatizo.

**Ete- Juwata Jazz Band**

Ni wimbo wa Juwata Jazz Band ambao nao ni wa mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Ete ni msichana aliyeolewa na kumkuta mwanamke mwenzake. Baadhi ya shoga zake walimkanya hakusikia.

Kilichotokea ni kwamba mke mkubwa akamwendea kwa mganga wa kienyeji na kumfanyia vitendo vya kishirikina. Ete yakamfika maswahibu, akaanza kuumwa maradhi yasiyojulikana, kiasi akarudishwa kwao.

Hapo sasa mashoga zake wakawa wamekusanyika na kumkumbusha jinsi walivyomkanya mwanzo na kumtaka aachane na mwanaume huyo ili alinde uhai wake.

**Matatizo ya Uke wenza-DDC Mlimani Park**

Wimbo huu wa DDC Mlimani Park Orchestra uliotoka katikati ya miaka ya 1980, unamzungumzia juu ya mwanamke mmoja anayemlalamikia mumewe aliyeoa mke wa pili.

Awali alikataa, lakini alihakikishiwa kuwa hatonyanyasika. Mambo hayakuwa hivyo. Mume amekuwa kama amemtelekeza. Mwanamke anapopiga simu ofisini kwa mumewe opereta anapokea na kumjibu maneno ya kejeli, halafu simu inakatwa. Unajua tena wakati huo simu za mkononi hazikuwapo. Ni lazima upige simu halafu opereta wa posta na wa ofisi wapokee, uunganishwe.

Mwanamke alipopeleleza akagundua kuwa yule opereta ndiyo mke wa pili wa mumewe. Sasa mke anamlalamikia mumewe na kumkumbusha kuwa alishasema tangu mwanzo, ukwe wenza ni majuto na kweli imekuwa hivyo.

**Penzi Haligawanyiki-Vijana Jazz**

Ni wimbo uliorekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1990, utunzi wa Hemed Maneti, ukiimbwa na mwanamama Kida Waziri. Unamhusu mwanamke mmoja anayemlalamikia mumewe kuwa alimruhusu kuona mke wa pili, lakini sasa penzi limeelemea kwa mke mwenzake.

Mwanamama huyo anakiri kuwa unaweza kugawanya mali na shamba, lakini si penzi, lazima lielemee kwa mtu mmoja.

**Uke Wenza-Tomatoma Band**

Ni wimbo wa katikati ya miaka ya 1980, mwanamke akilalamika kuwa ameolewa uke wenza, lakini tatizo ni watoto wa mke wenzake wanavyomfanya. Hawamheshimu kama mama yao na kumfanyia kila aina ya vituko.

# Kwetu Uswazi; Pinduapindua Uswahilini

Na Adam Fungamwango

KATIKA jamii yetu wakati mwingine kuna mambo ya ajabu sana. Hii huwezi kusema uswahilini tu. Ni kwamba kuna vitu ambavyo mtu akikusimulia unaweza ukadhani kuwa ni hadithi tu na hazina ukweli wowote.

Kwenye filamu hii ya 'Kwetu Uswazi' kuna vitu ambavyo vinaweza kukuacha mdomo wazi, ukadhani kuwa ni mtunzi tu ameongeza chumvi. Lakini ni kweli kwenye baadhi ya jamii zetu kuna vitu kama hivi vinatokea.

Filamu hii imechanganyika na ucheshi kidogo kutokana na aina ya waigizaji aliogiza kama kina mzee Majuto na mzee Jengua ambaye wote ni marehemu. Pia kwenye filamu yupo mzee Msisiri. Inaanza kwa kuonyesha kuwa mzee Majuto na kijana wake Kinye Mkali wakizozana kutokana na wote kuwa na tabia mbaya ya kuchukua wanawake ovyo.

Imefikia wakati wanawake wa mzee Majuto ndiyo hao hao wa kijana wake Kinye Mkali, hivyo kuanza kuzozana wenyewe kwa wenyewe.

Jirani yao mmoja mlevi anafika nyumbani kwa mzee Majuto na kumuonya juu ya kutembea na mkewe.

Mkewe Majuto naye anakwenda nyumbani kwa mke wa mlevi huyo na kumpiga mkwara juu ya kutembea na mumewe.

Upande wa pili nako, mzee Msisiri ana wake wawili. Lakini wake zake hao wote wana uhusiano wa kimapenzi na kijana wa mzee Majuto, Kinye Mkali.

Habari hizo ikafika mpaka kwa mzee Msisiri mwenyewe kwa sababu walikuwa wakigombana mara kwa mara juu yake, na akaapa kumfanyia kitu kibaya.

Kwa mzee Jengua nako, wanaume kibao wanajitokeza kutaka kumposa binti yake, lakini anakataa.

Vijana wa kiume wakifika hapo, yeye anawatoa mbio.

Ikaja kufahamika kuwa mzee huyo ana uhusiano wa kimapenzi na binti yake.

Binti akaanza kuwa na kiburi kwa mama yake, huku mama akiwa hajui ni kwa sababu gani.

Siku moja shemeji wa mzee Jengua ambaye ni kaka wa mkewe, akawafuma laivu wakikumbatiana, akawa amepata jibu la kwa nini hataki binti aolewe. Mzee Msisiri anamfanyia mambo ya kishirikina Kinye Mkali na anaanza kuwa chizi.

Matatizo ya akili ya mtoto wa Majuto yanasababisha wake za mzee huyo kumrudia mumewe na kumuomba msamaha. Ni kwa sababu hawawezi tena kuwa na uhusiano na mtu mwenye afya ya akili.






# Michepuko ya Dr. Dre kuchunguzwa

NICOLE Young, ambaye alikuwa mke wa mwanamuziki wa Marekani, Dr.Dre, ameitaka Mahakama kufanya uchunguzi kama mtalaka wake huyo alikuwa akitoa matunzo kwa wanawake watatu ambao inadai ni wapenzi wake.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Young ameiomba korti ichunguze ikiwa mwanamuziki huyo ndiye anayehusika kuwatunza wanawake hao pamoja na kuwanunulia nyumba za kifahari wakati wakiwa ndani ya ndoa yao.

Dre na mkewe Nicole,walipeana talaka mwaka jana kwa tuhuma ya kutokuwa mwaminifu katika ndoa yao.

Young anadai anataka wanasheria wazungumze na mmoja wa wale wanaodaiwa kuwa alikuwa mchepuko wake ambaye alimpatia nyumba yenye thamani ya dola milioni 2.15.



## Lil Frosh apelekwa rumande

RAPA kutoka Nigeria, Sanni Goriola,ambaye anayejulikana kama Lil Frosh, amepelekwa rumande katika gereza la Ikoyi kutokana na madai ya unyanyasaji wa kijinsia.

Lil Frosh, anadaiwa kumshambulia mpenzi wake, Okeoghene Iyomaterie, mnamo mwaka 2020.

Kesi hiyo ambayo imefunguliwa katika mahakama ya Lagos, inasimamiwa na jumuiya ya Kimataifa ya Wanasheria Wanawake.

## Wizkid kumbe muoga kama kunguru

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria Ayodeji Balogun, maarufu kama Wizkid, amefichua sababu ya kukaa mbali na malumbano.

Kwenye mazungumzo ya hivi karibuni, wizki Kikid,amesema yeye anakuwa na tabia ya ukimya na hupenda kuthibitisha jambo na ndio sababu hachukui hatua wakati wowote anapokabiliana na mabishiano.

"Ni rahisi sana. Mtu mjinga tu ndiye atakayependa kujaribu kudhibitisha jambo na hata wakati huo, utagundua kuwa huwezi kumpendeza kila mtu, kwamba huwezi kuishi kwa maoni ya watu," amesema.





## Victoria ashtukia utapeli

MKONGWE katika filamu za Nollywood, Victoria Inyama, amemjia juu msanii mwenzake Uche Maduagwu, kuwa ni muongo na anayetaka umaarufu kwa kujitangaza kuwa anajihusisha mapenzi ya jinsia moja.

Hivi karibuni, Maduagwu alichapisha picha katika ukurasa wake wa Istagram na kutangaza yeye yupo katika jamii hiyo.

Baada ya kusambaa katika mitandao ya kijamii, Victoria alijitokeza na kumuita ni muongo na tapeli kwani anataka umaarufu kupitia tangazo hilo.

## Harryson kumuoa anayempenda

MSANII wa muziki kutoka Nigeria Harrysong,yupo katika hatua ya mwisho ya kufunga ndoa na mchumba wake Alexer Gopa.

Mwanamuziki huyo aliweka picha katika ukurasa wake wa Istagram zikiwaonyesha wawili hao wapo katika sherehe ya Send off.

"Yote yatatimia, naelekea katika muda sahihi Machi 27,katika tukio litakalofanyika jimbo la Warri delta,"ameandika.



MAKALA

# AU mfupa aliopewa Rais Tshisekedi kujifunza kutafuna

**Mwandishi Wetu**



VIONGOZI wa nchi zinazounda Umoja wa Afrika, (AU) wamemchagua Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuwa mwenyekiti wao mpya kwa kipindi cha mwaka.

Rais Tshisekedi **(pichani),** amechukua wadhifa huo kutoka kwa Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini.

Nafasi hiyo ya juu katika bara la Afrika, ameipata wakati wa mkutano wa 34 wa viongozi wakuu wa nchi walipokutana wiki iliyopita mjini Addis Ababa, nchini Ethiopia.

Katika kikao cha 34 mwaka jana, kiongozi huyo alichaguliwa na viongozi wenzake kushikilia nafasi hiyo.

Katika kujipa uzoefu mwaka jana Rais Tshisekedi, alifanya ziara kadhaa katika nchi mbalimbali katika kujiimarisha kidiplomasia.

**CHANGAMOTO NCHINI MWAKE**

Katika kujihakikishia wadhifa wake huo hauyumbishwa na migogoro ya ndani, Rais Tshisekedi ameanza mikakati wa kujimarisha kwa kuamua kuvunja ushirikiano kati yake na kiongozi wa zamani Joseph Kabila.

Mkakati wake huo unaonekana kufikia malengo baada ya kufanikiwa kuwang'oa madarakani Waziri Mkuu na Spika wa Bunge ambao ni wafuasi sugu wa Kabila.

Rais Tshisekedi anajua kwa kufanya hivyo atakuwa na uwezo wa kuongoza nchi yake na hata ikitokea migogoro kwa wanachama wa AU, itakuwa rahisi kusimamia na kutatua bila kunyooshewa kidole.

Hata hivyo, kuna masuala mazito ambayo bado hajafanikiwa kuyapatia ufumbuzi ikiwamo kurejesha usalama upande wa Mashariki mwa nchi yake na kutimiza ahadi alizotoa baada ya kuapishwa mwaka 2019.

Katika suala la usalama, DRC bado inahitaji uwepo wa vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa, unaojulikana kama MONUSCO.

Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayesimamia shughuli za kusimamia amani, Jean-Pierre Lacroix, amekiri mwaka 2020 ulikuwa mgumu katika shughuli za kusimamia amani nchini Congo.

Hata hivyo, mjumbe maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Leila Zerrougui, anasisitiza lengo la kuwaondosha wanajeshi lipo palepale wakati wa utakapowadia.

Kutokana na hali hiyo, Rais Tshisekedi, anachukua hatua ya kuziangukia nchi jirani kwa nia ya kujaribu kupunguza ghasia kutoka makundi ya waasi.

Uhusiano wa kidiplomasia unazidi kuimarika kati ya nchi yake na majirani zake Rwanda na Uganda, zilizosaidia kijeshi kumng'oa madarakani Mobutu Sese Seko.

Katika vita vya kati ya mwaka 1998 mpaka 2003 vilivyoitwa "vita vya pili vya Congo", viliyaingiza mataifa sita katika mapigano makali. Nchi za Angola, Zimbabwe, Namibia na Burundi zilibaki upande wa Kabila.

Kabla ya kuondoka madarakani kufuatia ushindi wa Tshisekedi, mtangulizi wake alianza mkakati wa kujenga uhusiano na mahasimu wake, Rais Paul Kagame wa Rwanda na Yoweri Museveni wa Uganda.

Rais Kagame amekuwa akishinikiza kuangamizwa kundi la waasi wa Kihutu (FDLR) walioko ndani ya Congo, huku Museveni akisisitiza utayari wake wa kuisaidia Congo, utakuwa kuwafyeka wapiganaji wa Allied Democratic Forces (ADF), ambao bado ni tishio kwa nchi zote mbili.

Maelewano kati ya Tshisekedi na Kagame yanazidi kuimarika, tayari kiongozi huyo wa Rwanda alifanya ziara DRC mwezi wa Juni mwaka 2019.

Hata hivyo, mtihani mzito unatokana na raia wengi wa Congo kuwa bado wana machungu kutokana na Rwanda kujihusisha kijeshi nchini humo miaka mingi ya nyuma.

Wakati Tshisekedi akirekebisha uhusiano wa Congo na Rwanda na Uganda, pia amechukua jukumu la kuwapatanisha majirani zake ambao nao wamekuwa katika mvutano wa kidiplomasia.

Mwaka jana akishirikiana na Rais wa Angola, João Lourenço, walifanikiwa kuitisha mkutano wa kilele mjini Luanda, ambao uliohudhuriwa na Kagame na Museveni kujadili njia za kuondoa tofauti zao.

Angola inaangaliwa kama kitovu cha nguvu ya kijeshi na kiuchumi.

Mvutano mwingine ambao unamnyima usingizi ni ule unaoendelea kufukuta kati ya Rwanda na Burundi.

Tangu jaribio la mapinduzi dhidi ya Rais wa zamani Pierre Nkurunziza, mwaka 2015. Burundi inaituhumu Rwanda kuwa nyuma ya mpango huo na pia inawapa hifadhi baadhi ya watuhumiwa.

Tshisekedi aliwaalika Kagame, Museveni, Ndiyishimiye na Lorenco, katika mkutano uliofanyika Goma, ukiwa na lengo la kujenga msingi wa kuaminiana na kutuliza uhasama.

Rais Tshisekedi anatambua umuhimu wa uhusiano mwema na majirani zake ili aweze kuwa na utulivu wa kisiasa.

**KIKWAZO KINGINE**

Mwenyekiti mpya wa Umoja wa Afrika, atakuwa na kazi ngumu kuyashughulikia masuala yanayoukabili Umoja huo wakati huu na ambayo mtangulizi wake Rais Ramaphosa, wa Afrika Kusini ameyaacha bila kupatikana kwa ufumbuzi.

Miongoni mwa vikwazo hivyo ni mauaji na mashambulio yayofanywa na vikundi vua kigaidi vyenye itikadi kali katika jimbo la kaskazini la Cabo Delgado nchini Msumbiji, Nigeria na Mali.

Pia mgogoro wa Libya ambao kujiingiza kwa dola za kigeni Ufaransa, Urusi na Uturuki kumeongeza kurudisha nyuma juhudi za upatanishi unaofanywa na Umoja wa Afrika.

Migogoro mingine ambayo kiongozi huyo atakabiliana nayo ni kurudisha amani nchini Somalia na kugawanyika kwa nchi wanachama kuhusu hatima ya Sahara Magharibi.

Mwenyekiti mpya kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake, ataukuta umoja huo na taasisi zake katika hali ile ile ya kushindwa kuwajibika ipasavyo.

Pia wakati wa uongozi wake ana kazi nzito ya kuhakikisha Bunge la Afrika lilioasisiwa 2004 linakuwa na nguvu kisheria katika nchi zote.

Bunge hilo lenye makao yake makuu, Afrika Kusini lilitarajiwa liwe jukwaa la kuchukua maamuzi kuhusu matatizo yanayolikabili bara hilo na kufanyiwa kazi na Halmashauri Kuu yenye makuu mjini Addis Ababa nchini Ethiopia.

Kwa bahati mbaya miaka 17 baada ya kuundwa bado halijakamilisha lengo hilo.

Wengi wanaamini Umoja wa Afrika hauna meno ya kuuma, hasa panapotokea ukandamizaji wa demokrasia na kuzorota kwa utawala bora miongoni mwa nchi wanachama.

Pamoja na yote, Tshisekedi kushika nafasi hiyo ya uenyekiti inairejesha Congo katika jukwaa la kimataifa na kuondoa ile sura ya muda mrefu kuwa taifa lenye misukosuko, utawala mbovu na vita.

Anatarajia angalau kuwa na mafanikio katika upande huo, hivyo anaweza kumjengea haiba katika siasa za Afrika na Kimataifa.

**KWA MASAADA WA MITANDAO**

MAKALA

# DARAJA JPM, LINAVYOBEBA HISTORIA YA MWENYE JINA, WENYEJI WAKAZI

## ● Ilikotoka huzuni, inakoelekea neema

**Na Rose Jacob, MWANZA**




Ndivyo ilivyo daraja la JPM, lililokwishaanza kujengwa mkoani Mwanza. **PICHA: MTANDAO.**

MWANZA ni mkoa unaoundwa na wilaya saba za Nyamagana, Ilemela, Ukerewe, Kwimba, na Magu na kuna wilaya za Misungwi na Sengerema zinazoetegemea usafiri ndani wa Ziwa Victoria, wananchi wake wakitegemea vivuko viwili; MV Misungwi na MV Sengerema.

Kuvuka ziwani hapo, pia kuna jumla ya magari 1,600 yanayochukua wastani wa saa mbili na nusu kuvuka ziwa, kutoka Kigongo kwenda Busisi na pana historia ya kupoteza maisha ya baadhi ya wavukaji ziwani.

**SIMULIZI YA JPM**

Serikali sasa inachukua hatua kujenga daraja kumaliza tatizo hilo, mwasisi Rais Dk. John Magufuli ana simulizi ya kunusurika, mkasa uliomfika miaka mingi, alipokuwa anatoka Busisi, kuelekea Mwanza.

"Nilipofika kwenye kivuko nakumbuka kilikuwa ni kivuko cha Ferry kati ya MV Geita au MV Sengerema, kilikuwa kimeharibika, yaani kilikuwa kinaharibika kila siku," anaeleza, kwamba aliposogea kwenye kivuko cha Busisi Kigongo, kulikuwapo mtumbwi unaovusha watu kwa hela, ikiwa desturi ya kila kivuko kinapoharibika.

Anaendelea: "Nilipokuwa hapo kwenye mwalo waliniambia wahusika niingie kwenye mtumbwi na pikipiki yangu wataingiza. Nikafikiria, moyo ukakata.

"Palikuwapo mtu alikuwa na familia yake na baiskeli wakapakiwa.Mimi nikazunguka Kamanga nilipofika Mwanza nikapata taarifa ule mtumbwi umezama na umeuwa watu 11."

Ni ushuhuda anaosema umemsukuma kujenga daraja la kumbukumbu ya vifo vya majini mahali hapo, kutokana na kukosekana usafiri sahihi, hata alipokuwa katika kampeni ya uchaguzi aliahidi kujenga daraja, japo kuna ambao hawakuamini kama angetekeleza.

Katika hilo sasa, Dk. Magufuli, anamtaka mkandarasi mjenzi wa daraja la Kigongo-Busisi kwa gharama ya Sh. bilioni 700, kampuni ya China Civil Engineering Group, kukamilisha mradi ndani ya miaka waliokubaliana.

**MENEJA TANROADS**

Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mwanza, Vedastus Maribe, anasema daraja hilo litaunganisha barabara kuu za Usagara, Sengerema na Geita katika Ziwa Victoria, ambazo pia ziko kwenye ushoroba wa Ziwa Victoria.

Anaainisha inaanzia Sirari mpakani Mwanza na Kenya hadi Mutukula mpakani na Uganda (Km.774); ushoroba ukiunganisha mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Geita, Kigoma na Kagera, pia nchi jirani; Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC), Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya.

Maribe anasema kukamilika kwa mradi, wanatarajia kuwapo mageuzi ya magari kuvuka kati ya Kigongo na Busisi kutoka saa mbili za sasa, hadi dakika nne na idadi ya magari yavukayo kuongzeka hadi 10,200 kwa siku.

Kwa mujibu wa Maribe, ni daraja lenye urefu mita 3,200 (Km 3.2) na upana mita 28.45 likitarajiwa kuwa refu kuliko yote aina hiyo Afrika Mashariki na la sita barani Afrika, nyuma ya yaliyoko nchi za Misri, Nigeria, kuvuka Mto Suez (Misri) na Msumbiji.

Umbile lake ni kwamba, litakuwa na njia mbili za magari zenye upana wa mita saba kila upande, njia ya waendao kwa miguu na maegesho ya dharura yenye upana wa mita tano kila upande.

Aidha, kunatajwa kuwapo barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 1.66, ambazo ni za kimkakati kimaendeleo kwa wananchi kukuza uchumi wao.

Usanifu wa daraja unatumia teknolojia ya madaraja marefu, utakaokuwa na nguzo kuu tatu zikiwa na kimo cha mita 40 na umbali wa mita 160 kati ya nguzo moja hadi nyingine.

Pia, anaeleza msingi wake utachimbiwa kimo cha mita 60 kutoka chini na barabara za magari zitakuwa na urefu wa mita 1,660; upande wa Kigongo mita 1,160 na Busisi mita 500.

Maribe anasema utekelezaji wa mradi huo ulioanza Februari mwaka jana, unatarajiwa kukamilika Februari 24 mwaka huu, unagharamiwa na serikali.

Mhandisi Mshauri wa Mradi, Abdulkarim Majuto, anasema janga la corona duniani ndilo lilichelewesha kuanza kwake, kutokana na kukwama wataalamu waliotoka nje.

**UKAGUZI UTEKELEZAJI**

Maribe anasema hadi sasa, ujenzi wa kambi ya mhandisi mshauri na mkandarasi umekamilika, pia usimikaji mtambo wa kuchanganya zege pande zote, Kigongo na Busisi, madaraja ya muda na mahitaji kama eneo la kukunja vyuma, vifaa muhimu vikishashaletwa kwa wastani wa asilimia 93.

Anafafanua: "Mkandarasi ameishalipwa jumla ya Sh. milioni 87,508.604 ambazo ni malipo ya awali, mhandisi mshauri ameishalipwa Sh. milioni 1,437.127 ambazo ni malipo ya awali)."

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipokuwa ziarani katika daraja hilo, anasema ujenzi huo ni mwendelezo wa kujenga madaraja mengine, ambayo yataongeza maendeleo ya ukuaji uchumi Mwanza na kwingineko kwa kurahisisha usafiri .

Ni hoja inayoungwa mkono na wabunge wa Sengerema Hamiss Mwagawa na Alexandra Mnyeti wa Misungwi, wanaokiri ni ishara ya fursa za mji Misungwi na Sengerema wanakoandaa jumla ya viwanja 1,200 kwa ajili ya maegesho, yatakayochangia kukuza uchumi na kipato cha wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alipozungumza wakati alipokagua ujenzi wa daraja hilo, anathibitisha ulinzi umeimarika katika maeneo ya mradi na wananchi wako mstari wa mbele kuunga mkono .

"Jumla ya Sh. milioni 3,145.662 zimetumika kulipa fidia kwa watu na mali zilizoathiriwa na mradi huo, hadi sasa mradi wa ujenzi wa daraja la JPM umezalisha jumla ya ajira 416 ambapo asilimia 84 za waajiliwa ni Watanzania," anasema.

Wakazi wa Mwanza, wanasema daraja hilo ni ukombozi kwa wakazi wa Misungwi na Sengerema na taifa kwa jumla,

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamuriho, anaiagiza TANROADS kuhakikisha inatoa ajira ya miradi mikubwa kwa makandarasi wazawa, ili wajifunze na kupata ujuzi kutoka kwa makandarasi wakubwa wageni.

Katika ziara yake kwenye mradi, Mhandisi Chamuriho, anasema alikuta mtumishi mmoja tu mzawa anayeendesha mtambo katika ujenzi huo, hivyo akataka mikataba yote mikubwa ssa iwe na asilimia ya ushiriki wa moja kwa moja kwa makandarasi wazawa.

"Kampuni ya CCECC ipo nchini tangu mwaka 1967, lakini cha kushangaza hakuna mkandarasi aliyepata kujua kuendesha shughuli za ujenzi wa miradi mikubwa hapa Tanzania," akitaka miradi inayofuata itoe.

Pia, waziri anaagiza wananchi jirani na mradi wapewe ajira na wamekubaliana na wakurugenzi na viongozi na maofisa uhusiano wa kampuni, kufanya utaratibu wa kuwatambua wahitaji, ikiendana na malighafi yanayopatikana wilayani Misungwi zianze kununuliwa, baada ya kuhakikiwa ubora.

"Tumeongea na DC (Mkuu wa Wilaya) wa Misungwi Juma Sweda, naye ametoa changamoto zake, kuwa kuna matatizo aina ya benzonite (madini) yanatumika katika ujenzi wa daraja, lakini hayanunuliwi kwa wingi.

Waziri anasema, wamekubaliana kwamba mkandarasi atafiti kwa kushirikiana na mhandisi mshauri ili malighafi hayo yanayopatikana kwenye maeneo ya Misungwi yapimwe kwenye maabara za Shirika la Viwango la Taifa (TBS) kwa ajili yaa kutoa fursa zinunuliwe.

HABARI KIMATAIFA

# Miaka 100 jela kwa kuua ofisa polisi

**Kabale,** UGANDA

MAHAKAMA ya Wilaya Mbarara imewahukumu raia wawili kifungo cha miaka 100 gerezani, kwa kosa la kumuua ofisa wa polisi na kukimbia na silaha yake katika wilaya ya Kabale.

Mukwenda Mugisha (19) mkazi wa kijiji cha Gatete na Paul Dusingizimana (27), mkazi wa Manispaa ya Kabale, walihukumiwa Alhamisi.

Hata hivyo wawili hao waliomba huruma ya mahakama ya kuwapunguzia adhabu kwa kuwa walikuwa wamelewa walipokuwa wakitekeleza vitendo hivyo

Gazeti la Daily Monitor la Uganda limeripoti.

Mashtaka yaliyoongozwa na Luteni James Omondi, yaliyowasilishwa Januari 24, yalisema Mugisha na Dusingizimana walimshambulia na kumuua Gracious Byaryabakabu, aliyekuwa zamu ya kulinda Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Wilaya ya Kabale.

Walimpora silaha yake iliyokuwa na risasi takribani 30.

"Watuhumiwa hao pia walimpora Godfrey Tukamubona simu yake ya mkononi yenye thamani ya Sh. 60,000 baada ya kumsababishia madhara makubwa."

Mahakama pia ilielezwa kwamba mnamo Januari 29, wakiwa katika Gereza la Rutenga katika Manispaa ya Kabale, wawili hao walimtisha Patrick Arinaitwe kwa bunduki.

Aidha, walimteka nyara na kumwibia Sh. 20,000 zilizokuwa kwenye akaunti ya simu ya mkononi.

Watuhumiwa hao walikutwa na hatia ya makosa yote matatu ya unyang'anyi, mauaji na utekaji nyara.

**BBC**

## Kamanda wa Jeshi Rwanda afariki dunia

**Kigali,** RWANDA

ALIYEKUWA Mkuu wa Jeshi la Rwanda, Luteni Jenerali Jacques Musemakweli, amefariki kifo cha kawaida Alhamisi katika hospitali ya jeshi, kulingana na taarifa za kikosi cha ulinzi nchini humo.

"Ndio, Jenerali Musemakweli amefariki, alikuwa mgonjwa," ofisa mwandamizi wa jeshi la Rwanda aliiambia BBC.

Jenerali Musemakweli aliteuliwa kuwa mkuu wa ukaguzi wa Kikosi cha Ulinzi cha Rwanda, Novemba, mwaka 2019.

Hapo awali alishikilia nyadhifa za mkuu wa jeshi, mkuu wa walinzi wa rais na kamanda wa vikosi vya akiba.

Alikuwa mwanachama wa Rwandan Patriotic Front (RPF), kikosi cha waasi kilichoongozwa na Paul Kagame kilichoingia madarakani mwaka 1994.

**BBC**

## BBC yafungiwa kurusha matangazo

**Hongkong, CHINA**

CHINA imepiga marufuku matangazo ya BBC World nchini mwake.

Wadhibiti wa matangazo ya televisheni na redio walisema mwishoni mwa wiki.

China ilikosoa BBC kwa kutangaza taarifa za virusi vya corona na dhuluma dhidi ya kabila la walio wachache la Uighur.

BBC ilisema imesikitishwa na uamuzi huo.

Hatua hiyo inafuatia uamuzi wa mdhibiti wa vyombo vya habari Uingereza Ofcom kufutilia mbali leseni ya chombo cha habari cha China, Global Television Network (CGTN) kurusha matangazo yake nchini Uingereza.

Uamuzi wa Ofcom uliotolewa mapema mwezi huu baada ya kubaini kwamba leseni ya kituo cha CGTN ilikuwa inatumiwa visivyo na chombo cha habari cha Star China Media Ltd.



Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC), Fatou Bansouda, anatarajia kumaliza muda wake, Juni mwaka huu. Mwaka jana kutokana na misimamo yake mikali, Donald Trump alimzuia kuingia Marekani ikiwamo vikwazo vya fedha zake. **Picha/ BBC.**

## Bensouda wa ICC kupata mrithi wake Juni

**The Hague,** UHOLANZI

NCHI wanachama wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu, ICC wanatarajia kumchagua mwendesha mashtaka mkuu mpya kwa ajili ya mahakama hiyo.

Atakayechaguliwa atachukua nafasi ya kiongozi wa sasa aliyewekewa vikwazo na Marekani, Fatou Bensouda.

Wagombea wanne kutoka Uingereza, Ireland, Italia na Uhispania wanawania kuchukua nafasi ya mwendesha mashtaka anayemaliza muda wake, Bensouda.

Bensouda aliwahi kuendesha uchunguzi mzozo wa Israel na Palestina pamoja na Afghanistan.

Vyombo vya habari vya Uingereza vilisema kuwa Karim Khan kutoka Uingereza anaonekana kuwa katika nafasi nzuri akiwa mbele ya Carlos Castresana kutoka Uhispania, Fergal Gaynor wa Ireland na Francesco Lo Voi wa Italia.

Uchaguzi baada ya majaribio kadhaa nchi wanachama wa ICC, zilishindwa kufikia makubaliano, licha ya majaribio kadhaa katika wiki za hivi karibuni na sasa watamchagua mwendesha mashtaka mkuu wa mahakama hiyo katika uchaguzi utakaofanyika mjini New York, Marekani.

Bensouda, raia wa Gambia anatarajiwa kumaliza muda wake, Juni 15, mwaka huu, baada ya kuiongoza mahakama ya ICC iliyoko mjini The Hague, Uholanzi kwa miaka tisa.

Alikumbana na changamoto kubwa katika kazi za mahakama ya kimataifa, huku akiwa na rekodi tofauti za mafanikio.

**DW**

## Waziri wa zamani wa Myanmar akamatwa

**Naypyidaw, MYANMAR**

MWANACHAMA wa Baraza la Mawaziri la serikali iliyopinduliwa Myanmar, amewekwa kizuizini. Kyaw Tint Swe, ambaye ni mwanachama wa baraza hilo, iliyoondolewa madarakani baada ya mapinduzi ya kijeshi nchini Myanmar, ameripotiwa kukamatwa.

Katika taarifa iliyotolewa na Chama cha Kitaifa cha Kidemokrasia (NLD) kinachoongozwa na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Kiongozi halali wa nchi hiyo, Aung San Suu Kyi, iliripotiwa kuwa Swe, ambaye alikuwa kwenye baraza la mawaziri, alizuiliwa usiku wa manane pamoja na watu wanne waliokuwa naye.

Hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na serikali ya mapinduzi ya kijeshi kuhusu kukamatwa kwa waziri wa zamani Swe.

Mbunge Win Htein, ambaye ni mwanachama mwandamizi wa NLD, pia alikamatwa mnamo Februari 5, mwaka huu.

Jeshi la Myanmar liliipindua serikali ya utawala mnamo Februari Mosi, mwaka huu, baada ya vikundi vya kisiasa vilivyo karibu kudai udanganyifu ulikuwapo uchaguzi wa Novemba 8, mwaka jana na mvutano kuongezeka nchini humo.

Maofisa wengi na viongozi wa chama tawala ikiwamo Suu Kyi, walikamatwa.

Jumuiya ya Kimataifa, hasa Umoja wa Mataifa (UN) na Jumuiya ya Ulaya (EU), walilaani mapinduzi hayo.

Marekani imeweka vikwazo nchini Myanmar, huku watu wakiendelea na maandamano kudai kurudishwa kwa demokrasia tangu Februari 6, mwaka huu na polisi wakikabiliana nao katika maeneo mengi.

**TRT**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**TUNAUZA MAENEO MAZURI YANAYOFAA KWA KUJENGA SHELL (PETROL STATIONS):**

Wawasiliana na Tanlands Real Estate Agency (TREA).. Simu No: 0628 336 736 / 0759 848 155.

**VIWANJA 50 VILIVYOPIMWA VINAUZWA KIMBIJI - KIGAMBONI:**

Kigamboni City Mji wa Kitalii. Kununua Viwanja wasiliana na Njani Property Agency (NPC). Simu: 0657 990015

**NAFASI ZA KAZI**

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO...... OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RICHARD MWASENGO MWAKAJE**
**And**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LUSEKELO RICHARD MWAKAJE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before …. Day of …… 2021

Dated at Dodoma this 9th Day of February 2021.

Presented for filing this 11th day of February 2021.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ELIAS LUFWANDALI ERNEST** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 899 DDP TOYOTA BREVIS.** Chassis namba **JCG150003492.** Engine namba **1JZ0064578.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI: DAR/CHU/RB/80753/2021**

**TANGAZO LA KUPOTEA OFA YA KIWANJA**

**DEUS NHOGELO** MKAZI WA MAJENGO MANISPAA YA SHINYANGA.

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA NAMBA **101 KITALU "T"** MAJENGO MANISPAA YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA DEUS NHOGELO KWA SIMU NAMBA **0767555111.**

**RB NAMBA/SHY/RB/ 2021, CONTROL NAMBA 9910820477118**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 8

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Nimekwambia kazi yako ni ndogo sana. Kuua. Asilimia tisini tayari nimeshafanya mimi. Ni kwamba leo jioni marehemu mtarajiwa atakuwa anakunywa kwenye baa moja hivi mitaa ya Tandika. Huyo anapenda sana vimwana. Nimemwahidi kumletea mrembo wa shoka. Ni rafiki yangu na nitakwenda na wewe hadi pale. Ninachotaka ni kwamba baada ya kunywa, mtaelekea kwenye vyumba ya kulala vilivyomo kwenye baa hiyo. Humo muende na vinywaji vyenu, utamwekea dawa kwenye pombe na wewe kazi yako itakuwa imeisha."

"Ni dawa ya aina gani kaka?"

"Ni hii hapa." Martin alifungua droo na kutoa pakti moja nyeupe.

"Hii ni dawa kwa upande mwingine ni sumu. Hata ukiishika haina madhara, ila ikishaingia kwenye pombe inageuka kuwa sumu."

"Hawezi kunishtukia?"


"Atakuwa ameshalewa. Na wewe kwa sababu nia yako ni kumtilia sumu, sidhani kama utakunywa kwa kufakamia. Pia mimi nitakuwapo hapo, ingawa nikikukabidhi kwake nitadanganya kuwa naondoka kuna kazi nakwenda kufanya."

Ilikuwa bado kidogo, Mwanaidi aulize sababu ya kumuua mtu huyo, lakini akasita kwani, kazi aliyopewa ni kuua tu na si kuuliza sababu ya kuuawa kwa mtu huyo.

"Kitu cha kwanza kabisa ambacho kitafanyika tukitoka hapa ni kukupeleka saluni. Utakwenda kujipamba huko kwenye saluni za bei kubwa, siyo kama zile zenu au ile unayofanyia kazi kule Mburahati. Yaani nataka uonekane kama malaika. Tika akikuona achanganyikiwe. Tena na wewe ulivyokuwa mzuri, na watakavyokupamba, mbona atakufa vizuri tu."

"Mimi nimekubali, cha muhimu unihakikishie usalama tu." Mwanaidi aliongea kwa sauti ya chini akionekana kukubali, ingawa ilionekana kwa mbali kuwa ni shingo upande.

"Hilo halina neno, ila nakusisitizia tena. Sitaki lawama we mwanamke. Kwanza ukifika pale uchangamke. Usionyeshe kama kuna kitu unacho moyoni, au umelazimishwa kwenda pale. Kitendo chochote cha kushindwa




**Ghafla Mwanaidi alitokea tu kumchukia mtu huyo. Pamoja na kwamba alionekana kuwa yuko vizuri kipesa, lakini damu yake tu haikumpenda. Lakini huyo huyo aliyetokea kumchukia, ndiye anayetakiwa kwenda kumuua.**

kutekeleza jambo hili ni kwamba utakuwa tayari umeshajikatia tiketi ya kwenda ahera kuungana na mpenzi wako Burhan ili kwenda kujibu tuhuma za kwa nini ulimuua."

***************************

Ni kawaida ya kwenye baa zozote zile, kila mmoja anakuwa na shughuli. Kuna wanaokunywa pombe kwa makundi. Wapo wanaokunywa pombe wakiwa ni mtu na mpenzi wake. Hawa mara nyingi wanakuwa ni wawili wawili. Kuna wanaocheza muziki, ambao nao wamegawanyika makundi tofauti.

Wapo wanaocheza mmoja mmoja. Wengine wawili wawili, mtu na mpenzi wake. Wengine wanacheza kwa makundi, wakipangana mstari na kucheza kama wacheza shoo.

Kuna wanaocheza mchezo wa pool. Vile vile kuna wacheza kamari ambao nao wako kwenye sehemu yao ya dude la mashine.

Ndivyo ilivyokuwa kwenye baa ya Kafuma iliyopo Temeke jijini Dar es Salaam.

Wahati huo huo, kati ya watu waliongia ndani ya baa hiyo, wakiwa ni mwanaume mmoja aliyevaa suti na msichana mmoja mrembo.

Walionekana ni mtu na mpenzi wake. Walipendeza kwa jinsi walivyoonekana. Pamoja na kwamba walivyotembea walionekana kama mtu na mpenzi wake, lakini kila mtu alikuwa na lake moyoni.

Hawakuwa wengine. Ni Martin na Mwanaidi. Walielekea hadi eneo ambalo walitaka kufika.

Kulikuwa na meza pana, iliyozungukwa na vitu vinne. Lakini ilikuwa na mtu mmoja tu. Mnene mfupi, aliyekuwa na nywele nyingi kidogo.

"Karibuni." Aliwakaribisha.

"Ahsante Tika, leo nimekuletea kitu, umekiona?"

Tika aliangua kicheko. Kicheko cha furaha na uroho.

Ghafla Mwanaidi alitokea tu kumchukia mtu huyo. Pamoja na kwamba alionekana kuwa yuko vizuri kipesa, lakini damu yake tu haikumpenda. Lakini huyo huyo aliyetokea kumchukia, ndiye anayetakiwa kwenda kumuua.

"Sasa mimi nakuachia huyu demu. Mimi kuna sehemu nakwenda. Nadhani nitarudi baadaye kidogo." Martin aliaga.

Mwanaidi alijua kabisa kuwa haikuwa aga ya kawaida. Ni kwamba lengo nikumuachia nafasi Tika na baadaye watoke hapo kwenda kwenye moja ya vyumba vya kulala vya baa hiyo. Lengo ni kuutoa uhai wa mwanaume huyo, kama anavyohitaji Martin.

Tayari Mwanaidi alishapewa tahadhari kuwa atakuwa anaangaliwa na si kweli kwamba Martin ameondoka, badala yake yupo sehemu ambayo yeye atakuwa anawaona, lakini wao hawamuoni.

"Unaonaje mrembo tukahamia chumbani?" Ilikuwa ni sauti nene ya Tika, ikipenya masikioni mwa Mwanaidi. Alikubali kwa kichwa. Pamoja na kumchukia, Mwanaidi hakupenda kumuua, lakini amelazimika ili kuulinda uhai wake.

Safari yao iliishia kaunta, ambako walitakiwa kwanza kuwasilisha vitu walivyonavyo kwa ajili ya kukaguliwa.

"Samahani kwa sasa tumeambiwa ni lazima tusachi kwanza pochi, mikoba na vitu wanavyobeba wanaingia kwenye vyumba kwa sababu wengine wanakuwa na silaha, au vitu vya kuhatarisha wenzao, si mnakumbuka lile sakata la mtu kuuawa na mpenzi wake gesti lilivyotikisa?" Dada mmoja wa kaunta alisema huku akichukua mkoba wa Mwanaidi kwa ajili ya upekuzi.

Ni maneno yaliyomshtua Mwanaidi. Mwili wake ulitetemeka. Lakini hakuna yoyote aliyetambua hilo.

"Laiti angetambua kuwa anayemsema ni mimi?" Mwanaidi alijisemea kimoyomoyo.

Mwanaidi wakati mwingine huwa hapendi kabisa kukumbuka, au kukumbushwa tukio hilo ambalo limegharimu ustawi wa maisha yake, kiasi cha kutokuwa na amani na ndilo limezaa hadi hili la pili la kutakiwa kuua. Dakika moja baadaye alimrudishia na kuwakabidhi chumba. Kazi ilienda kama ilivyopangwa.

Tika alizidiwa na kinywaji. Kitu ambacho kilikuwa kinamuudhi zaidi Mwanaidi ni kupapaswa na mwanaume huyo. Hata hivyo alilazimika kukubali kwa ajili ya kutimiza jambo lake.

Hakutaka yafikie mwisho. Hakutaka ifikie hatua ya kulala na mwanaume huyo. Hivyo kitendo bila kuchelewa, alisubiri ameingia msalani ulio humo humo chumbani, aliingiza mkono kwenye mkoba wake na kutoa dawa alizoambiwa. Vilikuwa ni vidonge viwili ambavyo alivitumbukiza haraka kwenye glasi aliyokuwa akinywa Tika.

Aliporudi hata hakuongea kitu, alichukua glasi iliyokuwa na nusu bia, akaimimina kinywani.

Dakika 15 tu baadaye, Tika alikuwa anakoroma na kutoa mapovu kinywani.

Alikusanya vitu vyake na kuondoka taratibu. Lengo ilikuwa akimbie mji. Lakini akakumbukua kuwa polisi walimtaka asitoke nje ya mkoa wa Dar es Salaam kutokana na mauaji ya mpenzi wake Burhan.

Kwa hili lililotokea, aliaambiwa na Martin kuwa atamlinda kwa gharama yoyote ili asijulikane kama ni yeye ndiye aliyefanya hivyo. Kutokana na hilo hakudhani kuwa polisi watajua kama ni yeye aliyefanya hivyo kwa sababu hata alivyojipamba na kuvaa wigi, alifanya kila njia ili kujibadilisha mwonekano. Ni siri kati yake na Martin tu.

Pia alikumbuka kuwa kuna malipo ya pesa ambayo aliahidiwa kutokana na alichokifanya.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# WAKALA AFUNGUKA SARR ALIKARIBIA KUTUA LIVER




**LIVERPOOL,** England

WAKALA wa winga wa Watford, Ismaila Sarr, amesema usajili wa nyota huyo katika dirisha la Januari wa kuelekea Liverpool ulishindikana saa 11 kabla ya dirisha hilo kufungwa kutokana na matatizo ya kifedha.

Sarr mwenye umri wa miaka 22 kwa muda mrefu alikuwa akihusishwa kutua kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England tangu Watford waliposhuka daraja msimu wa 2019/20.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho nne kwa jina lake kwenye Ligi Kuu England.

Manchester United chini ya Ole Gunnar Solskjaer nao walionyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo.

Liverpool walitakiwa kulipa pauni milioni 40 ili kupata huduma ya mchezaji huyo, lakini mambo yalishindikana saa 11 baadaye kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha dogo la usajili.

Kwa mujibu wa Daily Mail, dili hilo lilikwisha kukamilika na pande zote kukubaliana tangu Septemba, mwaka jana.

Wakala wa Sarr, Thierno Seydi amedai Liverpool walisitisha ghafla mpango huo, wakati kila kitu kilikuwa kimeshaweka sawa.

"Liverpool walishafikia makubaliano ya kina kuhusiana na Sarr, lakini mambo yalibadilika dakika za mwisho," amesema Seydi akinukuliwa na Sky Sport.

# Lewandowski: Mafanikio ya Bayern ni ya dunia

**DOHA,** Qatar

MSHAMBULIAJI Robert Lewandowski, amedai mafanikio ya Bayern Munich sio tu maalum kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, bali ni kwa soka la dunia nzima.

Bayern iliifunga klabu ya Tigres bao 1-0 nchini Qatar juzi Alhamisi na kutwaa taji la Klabu Bingwa Dunia kwa mara ya pili katika historia yao.

Limekuwa taji la sita kwa Bayern Munich chini ya Hansi Flick baada ya msimu uliopita kutwaa Bundesliga, DFB-Pokal Ligi ya Mabingwa Ulaya UEFA, Super Cup na DFL-Supercup.


Lewandowski, ambaye alitwaa tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka wa kiume wa Dunia wa Fifa 2020, alikuwa nguzo ya ushindi huo wa Bayern Munich dhidi ya Tigres kutoka Amerika Kusini, huku bao pekee kwenye mchezo huo likifungwa na Benjamin Pavard.


"Mataji sita ni kitu maalumu, ni habari kubwa sio tu kwa Bayern Munich, kwa ulimwengu wote wa soka," alisema Lewandowski akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa namna tulivyocheza, hiyo itabakia kwa muda, muda mrefu sana."

Bayern ni timu ya kwanza tangu Barcelona chini ya Pep Guardiola mwaka 2009, kushinda mataji yote bila kuruhusu bao.

"Hongera kwa timu yangu, wamefanikiwa kwa kitu kizuri kwenye historia, taji lao la sita," alisema Flick.



# *Eriksen kupishana na Jorginho Chelsea*

**LONDON,** England

CHELSEA imeripotiwa inaangalia uwezekano wa kumrudisha, Christian Eriksen kwenye Ligi Kuu England na kumpeleka, Jorginho Inter Milan kama sehemu ya dili la usajili.

Uhamisho huo utashuhudia kwa mara nyingine shujaa huyo wa zamani wa Tottenham, Eriksen akisajiliwa kwa wapizani wao wa zamani, huku Jorginho akirudi kwenye Serie A.

Chelsea tayari imefanya mawasiliano na Inter - inayonolewa na Antonio Conte, kwa ajili ya kumsajili Eriksen kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa gazeti la nchini Italia la Calciomercato.

Inter imekuwa ikihusishwa na Jorginho kwa muda, baada ya raia huyo wa Italia kukosa nafasi pale Stamford Bridge chini ya kocha aliyefukuzwa, Frank Lampard.

Ikiwa inajulikana Inter wanahitaji sana Jorginho na Conte anataka kumtumia kwenye mfumo wake pale San Siro.Inadaiwa kwamba, Chelsea iliyopo chini ya kocha, Thomas Tuchel inataka kiasi cha angalau pauni milioni 18 ili kumwachia nyota huyo.

Eriksen raia wa Denmark kesho Jumapili atatimiza umri wa miaka 29, huku Jorginho atakuwa na umri wa miaka 30 mwishoni mwa mwaka huu.

Klabu hizo mbili zipo kwenye mazungumzo ya kukamilisha dili hilo haraka inavyowezekakana.

## HABARI MICHEZO

# Lukaku anaweza kumsaidia Guardiola

**MANCHESTER,** England

ROMELU Lukaku angekuwa "msaada mkubwa" kwa Manchester City, kwa mujibu wa nyota wa zamani wa klabu hiyo, Elano.

Sergio Aguero amekuwa nje ya dimba kwa muda mefu wa msimu huu, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 akisumbuliwana majeruhi ya mara kwa mara.

Mkataba wa Aguero unamalizika mwishoni mwa msimu huu 2020-21 na bado mazungumzo ya mkataba mpya hayajaanza, huku Gabriel Jesus pia akihangaika kupata nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Pep Guardiola baada ya kukosekana kwa raia huyo wa Argentina.

Huku Aguero akiwa amecheza mechi tano tu za Ligi Kuu England na kuanza mbili na kushindwa kufunga au kutoa pasi ya mwisho msimu huu, Jesus amefunga mara nne na kutengeneza pasi za mwisho mbili katika mechi 14, kati ya hizo michezo 10 alianza.

Na sasa Elano anaona Lukaku mwenye umri wa miaka 27 akitua katika kikosi hicho angekuwa msaada mkubwa zaidi kwa Guardiola hasa kwa staili yake ya uchezaji.

"Wakati unapocheza kwenye daraja la juu, kwenye klabu kubwa na mashindano makubwa na una mtu kama Lukaku unakuwa na mafanikio makubwa sana," amesema Elano akinukuliwa na Daily Mail.

"Lukaku sio tu anatakiwa na City, lakini na klabu zote kubwa, kwa sababu staili yake ya uchezaji anaweza kuisaidia sana timu kufunga mabao," amesema Elano aliyeichezea City kati ya mwaka 2007 na 2009.






# MAGUIRE SIO KIONGOZI UTD - PARKER

**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire "sio kiongozi" na Ole Gunnar Solskjaer anatakiwa kutafuta nahodha mpya, amesema mlinzi wa zamani wa Manchester United, Paul Parker.

Mshindi huyo mara mbili wa Kombe la Ligi Kuu England amesema mlinzi huyo ameshindwa kuonyesha thamani yake ya pauni milioni 80 alizosajiliwa katika kikosi hicho.

United wanataka kumsajili mlinzi wa muda mrefu wa kucheza pamoja na Maguire, lakini Parker anaamini kuna tatizo kubwa kuhusu majaliwa ya nyota huyo kwa umuhimu wake kwa timu.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 56, ameliambia gazeti la Sun: "Licha ya nafasi ya Manchester United iliyopo kwenye Ligi Kuu, wanahitaji kujiimarisha kwenye soko la usajili la kipindi cha majira ya joto.

"Kuhusu beki wa kati, watu wanazungumzia kuhusu kumleta 'patina' wa Harry Maguire, lakini mimi naona wangeletwa mabeki wawili wa kati, kwanini isiwe aletwe mchezaji anayeweza kucheza na Victor Lindelof?

"Harry Maguire sio kiongozi, anacheza mchezo kwa ajili yake mwenyewe, anakaa sana nyuma, hata kupiga chenga hajui na anakimbia bila akili.

# *Gatusso hajui hatima yake*

**NAPPLES,** Italia

KOCHA wa Napoli, Gennaro Gattuso, amesema kuwa hajui ikiwa mechi yake dhidi ya Juventus ya leo Jumamosi itaamua hatima ya kibarua chake.

Baada ya kuondolewa kwenye Coppa Italia na Atalanta Jumatano iliyopita, kocha huyo alikiri vijana wake walipambana katika kipindi cha kwanza, lakini hakufurahishwa na shauku ya wachezaji wake katika dakika 45 za mwisho.

Mechi hiyo ya Coppa Italia ilimalizika kwa Napoli kuchapwa mabao 3-1 na mchezo unaofuata ni wa Serie A, ambao wanakutana na vigogo hao.

Ripoti nchini Italia zinadai mechi ya leo inaweza kuwa mechi itakayoamua hatima ya kocha huyo wa zamani wa Milan, lakini Gattuso amesisitiza hafikirii mchezo wa kombe unaweza kushinikiza uamuzi.

"Sijui, lazima uulize klabu, nahodha wa meli ni mimi, wakati mambo yanakwenda vibaya, na inamgharimu nahodha. Siwezi kufikiria hii kama suluhisho au mwisho, lazima nifanye kazi na lazima niweze kuamini. Mimi ni kocha, ni hivyo," amesema Gattuso akiiambia Sky Sport Italia.

Gattuso anaamini yeye hatakuwa kocha wa kwanza na wa mwisho na klabu ya Napoli, lakini kwa nafasi yake anapaswa kuhakikisha anajaribu kuiweka klabu kwenye mstari hadi jitihada zake zitakapoishia.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR KUIKOSA BARCELONA UEFA

●●● Ni baada ya mshambuliaji huyo Brazil kuumia paja na madaktari wasema atakuwa nje...

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR ataikosa Barcelona katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 utakaochezwa kwenye dimba la Nou Camp, baada ya kuumia kwenye mchezo dhidi ya Caen katikati ya wiki.

**Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Brazil atakuwa nje ya uwanja kwa wiki nne baada ya kuumia paja wakati wa mchezo wa ushindi wa Kombe la Ufaransa dhidi ya Caen, na hivyo kumfanya kutokuwapo pale Nou Camp kwenye mechi itakayofanyika Februari 16, mwaka huu.**

Pia yupo shakani kwenye mchezo wa marudiano utakaopigwa Machi 10, mwaka huu kwenye dimba la Parc des Princes, ambapo ni pigo kubwa kwa kocha, Mauricio Pochettino, ambaye tayari atamkosa Angel Di Maria kwenye mchezo wa huo wa nchini Hispania wiki ijayo.

PSG ilithibitisha juzi: "Neymar Jr ameumia paja la mguu wa kushoto Jumatano usiku. Baada ya vipimo na uchunguzi wa madaktari, hatakuwapo uwanjani kwa kipindi cha wiki nne."

Kwa mara ya mwisho klabu hizo kukutana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16, Neymar aliifungia mara mbili Barca wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 6-1 kwenye mchezo wa pili, na kupindua matokeo ya awali waliyoyapata PSG ya magoli 4-0 na kufuzu hatua iliyofuata katika msimu wa 2016-17.

Halafu baadaye Neymar akahamia PSG kipindi cha majira ya joto, baada ya Barca kutolewa kwenye robo fainali ya mashindano hayo na Juventus, kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 200, huku akiripotiwa kupuuzia ushauri kutoka kwa wachezaji wenzake, Lionel Messi na Luis Suarez.

Barcelona imekuwa ikijaribu kumrudisha Neymar pale Nou Camp tangu hapo, lakini dili hilo halijafanikiwa na sasa Messi majaliwa yake pale Barcelona hayajulikani, huku PSG wakitaka kumsajili kama mchezaji huru kipindi cha majira ya joto mara mkataba wake utakapomalizika.

## ZISIKUPITE

### MOURINHO YUKO SALAMA

NAFASI ya kocha, Jose Mourinho pale Tottenham Hotspur ni salama licha ya matokeo mabaya na tetesi za mashaka kutoka kwa wachezaji wakubwa. ***(Mirror)***

### MILAN, JUVE VITANI

KLABU ya AC Milan na Juventus zote za Italia zinamfuatilia kwa karibu winga wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 27. ***(Calciomercato)***

### DAMSGAARD AGEUKA DILI

LEEDS United, Southampton na West Ham United zinachuana na Tottenham Hotspur kuwania saini ya kiungo wa kati wa Sampdoria ambaye ni raia wa Denmark, Mikkel Damsgaard, 20. ***(Star)***

### ARSENAL ILIMSHINDWA PUIG

ARSENAL walishindwa kufanya uhamisho wa mkopo kwa kiungo wa Hispania, Riqui Puig mwenye umri wa miaka 21, kabla ya kumpata kiungo wa kati wa Real Madrid na Norway, Martin Odegaard (22). ***(Express)***

### LOVREN: SALAH HAONDOKI

MLINZI wa Zenit St Petersburg, Dejan Lovren, 31, anaamini rafiki yake wa karibu na mchezaji mwenza wa zamani wa Liverpool, Mohamed Salah, atakuwa Anfield kwa miaka mingi zaidi. ***(Talksport)***

### CAVANI HAKIJAELEWEKA

KLABU ya Manchester United bado haijaamua kama itaongeza mkataba wa mwaka mmoja kwa mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani, 34 na kiungo wa Hispania, Juan Mata (32). ***(Manchester Evening News)***

### ROMERO SAFARI IMEIVA

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Argentina, Sergio Romero (33), ambaye sasa ni chaguo la tano katika kikosi cha Manchester United ataachiwa kuondoka katika klabu hiyo kwenye kipindi cha majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

### FOSU-MENSAH ALIJITAMBUA

MLINZI wa Uholanzi na Bayer Leverkusen, Timothy Fosu-Mensah, 22, amekubali alilazimika kuondoka katika kikosi cha Manchester United ili kupata nafasi ya kuendeleza kipaji chake.***(Mail)***

### SKIPP KUULA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inatafuta jukumu muhimu kwa kiungo wa England, Oliver Skipp, 20, katika kikosi cha kwanza msimu ujao baada ya kucheza kwa mkopo Norwich City. ***(Football Insider)***

### MINO KIMYA KIMYA

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola amesema "lazima afanye kazi kimya kimya" linapokuja suala la kiungo huyo wa Manchester United ambaye ana umri wa miaka 27, huku kukiwa na ripoti zinazomhusisha na kurudi Juventus. ***(Talksport)***

HABARI MICHEZO

# Maxime ajipanga kuinusuru Kagera

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kuambulia sare ya bao 1-1 dhidi ya Gwambina FC, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema hataki kurudia makosa ya msimu uliopita kwa kucheza kwa presha katika mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Maxime alisema ili kuepuka kucheza mechi za 'Play off' ameandaa mikakati ya kutopoteza pointi katika kila mechi watakayocheza ili kumaliza katika nafasi saba za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Maxime alisema hakuanza msimu huu lakini hajakata tamaa ya kufikia malengo ya kuibakisha timu hiyo katika Ligi Kuu Tanzania Bara na anaamini watafanikiwa.

"Tumeona makosa ya mechi zilizopita na kuyafanyia kazi ili kuhakikisha mechi zetu zijazo tunavuna pointi muhimu katika mechi zilizopo mbele yetu," Maxime aliongeza.

Alisema mechi zote msimu huu zina ushindani na ni ngumu kwa sababu kila timu imejipanga na imejiimarisha kumaliza vyema katika hatua hii ya lala salama.

"Tunapambana kuhakikisha tunapata pointi muhimu katika mechi iliyopo mbele yetu kwa ajili ya kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi, ingawa tunajua si kazi nyepesi," aliongeza kocha huyo.

# Kikapu Zanzibar kuanza Jumanne

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Mpira wa Kikapu Zanzibar imepangwa kufanyika kuanzia Februari 16, mwaka huu Visiwani hapa.

Ligi Kuu hiyo itachezwa kwa mtindo wa Kanda ya Unguja na Pemba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Kikapu Zanzibar (BAZA), Rashid Hamza, alisema ligi hiyo inatarajiwa kushirikisha timu 12 za Unguja na timu 10 kutoka Pemba.

Hamza alizitaja timu hizo za Unguja za wanaume ni pamoja na Polisi, JKU, Nyuki, Stone Town, African Magic, Usolo na Milenium huku za wanawake zikiwa ni Zimamoto, JKU, KVZ na New West.

Alisema Kanda ya Pemba kwa upande wa wanaume itawakilishwa na Tonado, ABC, Michungwani, Calfonia, Clikers, Dolphine na Micheweni huku kwa upande wa wanawake ni Wete Stars na Chakechake Stars.

"Maandalizi yote muhimu kuelekea ligi hiyo yamekamilika na ratiba rasmi inatarajiwa kutolewa kesho (leo) Jumamosi," alisema Hamza.

Kiongozi huyo amewataka mashabiki wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi katika viwanja ambapo ligi hiyo itachezwa ili kutoa hamasa kwa timu kuonyesha ushindani.

# MGUNDA AFICHUA SIRI KILICHOIMALIZA AZAM

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema ushindi wa mabao 2-1 ambao timu yake imeupata dhidi ya Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa juzi jijini Tanga umetokana na kutumia 'mbinu' alizorejea nazo kutoka Cameroon.

**Mgunda ni Kocha Msaidizi wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo hivi karibuni ilikuwa Cameroon ikishiriki Fainali Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), lakini iliishia hatua ya makundi.**

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Mgunda alisema matokeo ambayo timu yake hayakutarajiwa na mashabiki wengi kufuatia kiwango ilichokionyesha Azam wakati ilipokutana na mabingwa watetezi, Simba wiki iliyopita kwa kutoka sare ya mabao 2-2.

"Ni kweli kuna vitu nimejifunza kutoka Cameroon kwenye michuano ya CHAN na nimewapa vijana wangu na sasa wanavifanyia kazi, kwa hiyo nadhani kikosi changu kinaimarika si kama kile cha mzunguko wa kwanza," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema mbali na 'madini' aliyoyapata nchini Cameroon kutokana na kuangalia baadhi ya timu zikicheza na kuchukua mbinu, lakini usajili wa wachezaji wapya katika dirisha dogo umekiimarisha kikosi chake.

"Usajili wa dirisha dogo nao umechangia sana sisi kushinda mechi hii, tumeingiza wachezaji tunaowahitaji na zile sehemu zote ambazo zilikuwa na upungufu kwa kiasi fulani tumefanikiwa kuziba," alisema Mgunda.

Hata hivyo alikiri mechi hiyo ya raundi ya 19 ilikuwa ngumu na yenye ushindani, lakini walifanikiwa vyema kutumia baadhi ya makosa ya wachezaji wa Azam na kuondoka na pointi tatu.

Ushindi huo wa juzi umeifanya Coastal Union kufikisha pointi 23 na kupanda hadi nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu Bara huku Azam yenye pointi 33 bado iking'ang'ania nafasi ya tatu.

Coastal Union itashuka tena dimbani Jumatano kuwakabili wenyeji Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena leo kwa Mbeya City kuwakaribisha vinara Yanga kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine na Mwadui FC kuvaana na Biashara United kwenye Uwanja wa Mwadui Complex mkoani Shinyanga.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (mwenye shati la kitenge), akikabidhi bendera ya Tanzania kwa wachezaji na viongozi wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), ambayo iliondoka nchini jana kuelekea Mauritania kwenye fainali za Afrika za U-20. **PICHA: TFF**

# *Soka la kukamia laiponza Azam FC*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema matokeo mabaya ambao timu yake inapata katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara yanasababishwa na wachezaji 'kukamia sana kichwani' badala ya kucheza mpira kama walivyoelekezwa.

Vivier ametoa kauli hiyo baada ya Azam kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Coastal Union na wiki iliyopita ikilazimisha sare ya magoli 2-2 na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba ya jijini Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema wameshindwa kuvuna pointi tatu katika mechi hizo mbili kwa sababu wachezaji wao wameweka mawazo tofauti kwenye akili zao badala ya kupambana uwanjani kusaka ushindi.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi za kufunga katika mechi dhidi ya Coastal Union, Simba, Namungo FC na Ruvu Shooting, lakini nafasi hizo walishindwa kuzitumia kutokana na kupoteza umakini.

"Hiyo michezo yote tumepata pointi mmoja, tulikuwa na uwezo wa kupata pointi tatu, ukiangalia dhidi ya Coastal Union, wachezaji hawakutuliza akili na kucheza kwa kukamia zaidi, hutakiwi kucheza mpira hivyo, wanatakiwa kutuliza akili," alisema Vivier.

Aliongeza sasa wataendelea kupambana kuhakikisha tatizo hilo linamalizika na baadaye kufanya vizuri kwenye mechi zinazofuata ili kufikia malengo yao kutwaa ubingwa wa msimu huu.

"Bado tuna nafasi ya kufanikiwa katika jambo letu, kwa sababu bado ligi inaendelea na sasa tunafanyia kazi upungufu wetu uliyojitokeza katika michezo iliyopita," alisema Vivier.

Azam FC ipo katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 33 imecheza michezo 19, Simba yenye pointi 39 iko juu yake, lakini imeshuka dimbani mara 17 na Yanga yenye pointi 44 ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 18.

Michezo
Jumamosi Februari 13, 2021
Nipashe




## Eriksen kupishana na Jorginho Chelsea

## Wazawa wapewe nafasi Taifa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutangaza kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, wadau wamelitaka shirikisho hilo kutoa nafasi kwa makocha Watanzania.

Hata hivyo, tayari tetesi zinamtaja Kim Poulsen, raia wa Denmark na kocha wa zamani wa timu za taifa za vijana anakaribia kurithi mikoba ya Ndayiragije.

Kiungo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars, Ally Mayai, amesema umefika wakati TFF ikawaamini makocha wa hapa nyumbani hasa katika kikosi kinachoshiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Mayai alisema kwa kutoa nafasi kwa wazawa kuifundisha Taifa Stars, itawasaidia makocha hao kupanda viwango na kuongeza uzoefu wa kushiriki mashindano makubwa.

"Ifike wakati TFF iwaamini makocha wazawa katika kuwapa majukumu ya kuiono Stars hasa kikosi kinachoshiriki fainali za CHAN ili nao waweze kupanda viwango kama Tanzania inavyowapandisha makocha wa kigeni wanaokuja kufanya kazi hapa nchini," Mayai alisema.

Mchezaji mwingine wa zamani wa timu hiyo (jina tunalihifadhi), alisema TFF imefanya haraka kuachana na kocha huyo ambaye anaonekana alikuwa na 'bahati' na Tanzania.

"Kwangu naona wamefanya haraka, hakustahili kuondolewa sasa, wasihangaike sana na kutimua makocha, wajiweke sawa kwenye kuimarisha misingi," alisema nyota huyo.

TFF ilitangaza kuachana na Ndayiragije ikiwa ni siku chake baada ya kurejea nchini kufuatia kutolewa mapema katika fainali za CHAN.

Mrundi huyo alianza fainali za CHAN kwa kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Zambia halafu akashinda goli 1-0 dhidi ya Namibia na mechi yake ya mwisho ya Kundi D alitoka sare ya magoli 2-2 ambayo iliwavusha wapinzani wao Guinea na kwenda hatua iliyofuata.

# YANGA 'KUVUNJA MWIKO' MBEYA

## Haijapata ushindi dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine tangu ...

**Na Adam Fungamwango**

TUMEFUATA ushindi, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Mbeya City itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Yanga itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu na kutopata ushindi katika mechi ya msimu uliopita kwenye uwanja huo.

Pamoja na kwamba Yanga iliifunga Mbeya City kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Saalam bao 1-0, Septemba 13, mwaka, vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wataingia uwanjani wakiwa na rekodi ya kutoshinda mechi dhidi ya timu hiyo tangu iliposhinda mabao 2-1 katika msimu wa 2018/19, kwa mabao ya Heritier Makambo ambaye kwa sasa anaichezea Horoya FC ya Guinea.

Hata hivyo, msimu huu Yanga inaonekana imekamilika kila idara, ikiwa na wachezaji wapya wenye viwango vya juu kama Tuisila Kisinda, Mukoko Tonombe, Michael Sarpong, Yacouba Songne, Kibwana Shomari, Yassin Mustapha na Fiston Abdulrazack.

Itakuwa ni mechi muhimu kwa pande zote mbili, kwani wakati Yanga ikitaka kupata pointi kwa ajili ya kuufukuzia ubingwa ambao haijaupata kwa misimu mitatu sasa, huku Mbeya City ikizitaka pointi tatu ili itoke katika eneo la hatari na kujiwekea mazingira mazuri ya kubakia Ligi Kuu.

Kaze alisema kikosi chake tayari kwa mechi hiyo na maandalizi yote muhimu yamefanyika kikamilifu.

"Tumekuja huku kwa ajili ya kutafuta pointi tatu kama tulivyofanya katika mechi zilizopita, tunataka kuendelea kushinda katika kila mchezo tutakaocheza, hii ndio njia kuu ya kufikia malengo yetu," alisema Kaze.

Ofisa Uhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema katika mechi ya leo watamkosa kiungo mshambuliaji, Saido Ntibazonkiza ambaye alibaki jijini kutokana na kutokuwa fiti kimchezo, lakini akiendelea na programu maalumu ya mazoezi.

"Tumejiandaa kupata pointi tatu, kwa hiyo tunawaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi ili kuwaongezea morali wachezaji wetu," alisema Nugaz.



Wachezaji wa Yanga kutoka kushoto, Mukoko Tonombe, Adeyum Saleh, Zawadi Mauya na Farid Mussa wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Mbeya City itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya. **PICHA: MTANDAO**.

Naye Meneja wa Mbeya City, Mwigane Yeya, aliliambia gazeti hili maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na wanaamini watavuna matokeo chanya chini ya usimamizi wa kocha wao Mganda Mathias Lule.

"Kikosi chetu kimerejea Mbeya na kimeiva baada ya kambi ya wiki tatu huko Rungwe kwenye mji mdogo wa Tukuyu," alisema mchezaji huyo wa zamani wa timu hiyo.

Yanga ndiyo timu pekee mpaka sasa haijapoteza mechi yoyote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikicheza mechi 18, kushinda mechi 13 na kutoa sare mechi tano, ikiwa kileleni baada ya kujikusanyia pointi 44 wakati Mbeya City kabla ya mechi za jana, ilikuwa inashika nafasi ya 17, ikicheza mechi 18, lakini ikiwa na pointi 14.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya Mwadui FC dhidi ya Biashara United kutoka Musoma itakayofanyika kwenye Uwanja wa Mwadui Complex mkoani Shinyanga.

Wakati huo huo Tanzania Prisons iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga, Rukwa jana mchana.

Jeremiah Juma aliifungia Tanzania Prisons mabao yote mawili dakika ya 29 na 50 wakati goli pekee la KMC lilipachikwa wavuni na Israel Mwenda dakika ya 67.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042